**Uchunguzi** tuhuma ubadhirifu bandari mbioni kukamilika

UKURASA 4



**Watu** 6 wafariki dunia katika ajali ya basi

UKURASA 4


Ukurasa 14
DENIS SASSOU-NGUESSO
Kashinda tena akianza safari ya miaka 41 urais, umri miaka 77

siasa
JUMATANO MACHI 31, 2021
Nipashe
HABARI BORA NA KAMILIFU

Ukurasa 13
JPM alivyopanua wigo wa uelewa katika namna ya kuongoza Afrika

## Jicho linavyoangazia 'hapa kazi' ya Rais mpya na ugeni Makamu wake

• Dk. Slaa: Niliwafahamu hivi miaka 25 na JPM

Sabato Kasika na Anthony Gervas, MWANZA

UYO ndiye Samia Suluhu Hassan Rais wa

Hayati Dk. John Magufuli, alipokuwa na Balozi Dk.Willibrod Slaa. **PICHA: MTANDAO**

**UTEUZI MAKAMU RAIS**

Vilevile, ni jana tu Rais Samia aliendelea kuonyesha kuwa anataka kufanya kazi na watu wa aina gani, baada ya kumpendekeza Dk. Philip Mpango kuwa Makamu wa Rais, akiamini ndiye anayeweza kumsaidia katika nafasi hiyo.

Dk. Mpango amekuwa Waziri wa Fedha kwa kipindi cha miaka mitano mfululizo tangu alipoteuliwa na Rais Hayati akiwa mbunge asiye na jimbo, Dk. John Magufuli na akamteua tena, baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka jana.

Jana saa 6.32, Spika wa Bunge Job Ndugai, alitangaza kupitishwa kwa asilimia 100, jambo ambalo mbali na kumtakatisha Dk. Mpango aliyeaga rasmi kwa kutoka bungeni jana saa 6.35 akiwa amevua ubunge wa Buhigwe kikatiba, vivyo hivyo kauvua uwaziri wa Fedha.

Samia Suluhu Hassan, aliyejionyesha rasmi kwa matendo kwamba yeye ni kiongozi wa aina gani, utendaji kazi wake na aina ya makundi watakaofanya kazi naye.

Hata pendekezo lake la uteule lina wasifu ambao Dk. Mpango aliwekeza, ikiwamo utiifu.

Binafsi anakiri wasifu aliyopewa bungeni wa 'upole' ila akataja sura yake ya pili iliyojificha ya ukali na huonekana pale anapokuwa katika jukumu la kumsaidia Rais Samia, anaona maslahi ya Tanzania yanachezewa.

Mhadhiri wa Chuo cha Diplomasia jijini Dar es Salaam, Abbas Mwalimu ni mchambuzi wa siasa, ana maoni yake kuwa:"Tayari mama Rais Samia Suluhu Hassan ameshatuma ujumbe wa kuwaondoa wasiwasi Watanzania kuwa Dk. Magufuli amemaliza kazi iliyomleta duniani ya kumwonyesha namna kazi zinavyofanywa."

Anafafanua, kwa sasa Rais huyo wa awamu ya sita, anajua namna ya kutekeleza na kuchukua uamuzi mgumu kwa maslahi ya taifa kwa kufuata njia hiyo ambayo Dk. Magufuli ameiacha.

INAENDELEA UK.12

UKURASA 11

Jumatano Machi 31, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580536

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US

# Bendera chuma, mlingoti chuma

• **Mpango** amrithi Samia, atema cheche kama bosi wake... *Ukurasa 2&3*







Makamu wa Rais Mteule, Dk. Philip Mpango, akizungumza baada ya jina lake kutangazwa na Spika, bungeni jijini Dodoma jana. **Picha ndogo:** Spika wa Bunge, Job Ndugai, akipokea bahasha yenye jina lililopendekezwa na Rais Samia Suluhu Hassan, kushika nafasi hiyo, huku Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mwanaidi Ali Khamisi (katikati), akitulizwa na wabunge wenzake, baada ya kuangua kilio kutokana na aliyekuwa waziri wake, Dk. Mpango, kuteuliwa kushika nafasi hiyo. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**




Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play

App Store

## Wadau: 'Viatu' vinamtosha

UK.3

**MICHEZO** **MIQUISSONE, KAGERE WAMTIBULIA GOMES** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA



Makamu Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Bara, Philip Mangula, akiongoza kikao cha Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya chama hicho Taifa, jijini Dodoma jana. Kulia kwake ni Makamu Mwenyekiti wa CCM Visiwani, Rais mstaafu wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, Mjumbe wa Kamati Kuu Rais Samia Suluhu Hassan na Mjumbe wa Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya CCM Taifa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Mwinyi. **PICHA: IKULU**

# Bendera chuma, mlingoti chuma

**Na Waandishi Wetu**

BENDERA chuma, mlingoti chuma. Ndivyo picha halisi inavyoonyesha katika dhamira za dhati za Rais Samia Suluhu Hassan na Makamu wa Rais Mteule, Dk. Philip Mpango.

Kwa maneno mengine, ni viongozi ambao kutokana na historia zao kiutendaji na kauli zao baada ya kuthibitishwa kushika nyadhifa hizo kwa nyakati tofauti, wanaonyesha kuwa ni watu wasiotikisika na hawatakuwa na msalie mtume kwa wale watakaopindisha sheria za nchi na wabadhirifu.

Wakati wa mazishi ya kitaifa ya aliyekuwa Rais wa Tanzania, Dk. John Magufuli, jijini Dodoma, Rais Samia alisema:

"Kwa wale ambao wana mashaka, 'mwanamke huyu ataweza kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania?' Nataka niwaambie aliyesimama hapa ni Rais... Nataka nirudie, aliyesimama hapa ni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambaye maumbile yake ni mwanamke."

Kauli hiyo ilionyesha kuwa ni mtu anayejiamini, mwenye uwezo na yuko tayari kushika wadhifa huo, tofauti na mitazamo ya baadhi ya watu waliokuwa na shaka kama anatosha kuvaa viatu vya urais. Makamu wa Rais mteule, Dk. Mpango, ameonyesha kuwa si mtu wa mzaha baada ya kuonya kuwa hatakuwa na uvumilivu dhidi ya wala rushwa na mafisadi wakati akitekeleza majukumu yake mapya.

Alizungumza hayo bungeni jana alipopewa nafasi ya kuaga na Spika Job Ndugai, dakika chache kabla ya kutangazwa kwa matokeo ya kura za wabunge waliopitisha jina lake kuwa Makamu wa Rais.

Mtaalamu huyo wa uchumi alisema kwa kuzingatia kwamba ametoka kwenye familia maskini, atahakikisha ndoto za Rais wa Awamu ya Tano, Hayati Dk. John Magufuli, za kuwainua wananchi wanyonge na maskini zinatimia.

"Nimevaa kiatu cha umaskini toka utoto wangu. Hata katika utumishi wangu Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM), nilijikita kwenye uchumi wa maendeleo.

"Wakati wa mazishi ya kitaifa ya Hayati Rais Magufuli, kuna matukio mawili yalinigusa sana. Moja, ni lile la Dar es Salaam pale wananchi wanyonge walipoamua kuruka ukuta wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere kumsindikiza kipenzi chao.

"Sasa, ndoto za wanyonge hawa lazima zimulikwe na zitimizwe, wanataka SGR (reli ya kisasa) ikamilike, bwawa la umeme likamilike, barabara za vijijini zikamilike, huduma za afya ziwe bora zaidi, maji, usalama ili waendelee kufanya kazi shughuli zao. Hawataki rushwa," alisema.

**ASEMA SI MPOLE**

Alisema katika uongozi wake ataendeleza ndoto za Hayati Rais Magufuli za kutaka Tanzania ipige hatua zaidi kiuchumi kwa kusimamia rasilimali zake, akihimiza kuwa rasilimali za nchi liwe jicho la kila Mtanzania.

"Ninajua wamesema mimi ni mpole, mimi ni mcha Mungu, ninajitahidi kumcha Mwenyezi Mungu kwa sababu bila hilo mimi si chochote.

"Lakini, kuna maeneo ninaomba muwe mnasema ukweli. Mimi siyo mpole kiasi hicho. Kwenye mambo ya ovyo ovyo, ya matumizi mabaya ya fedha za umma, hapana! Mimi siyo mpole. Kwa watu wanaokula rushwa, mimi siyo mpole.

"Na kwa hilo nitaomba mnisamehe pale ambapo itabidi kusimamia kazi za umma kwa ajili ya maendeleo ya Tanzania. Ninawaambieni ukweli, nitamsaidia Mheshimiwa Rais kwa kuhakikisha kwamba tunakwenda sawasawa," alisema.

Dk. Mpango alisema hali ya umaskini nchini bado ni kubwa, akibainisha kuwa zaidi ya watu milioni 14 wanaishi chini ya kiwango cha umaskini, akisisitiza kuwa haikubaliki.

Dk. Mapango pia aliahidi kuwa ataendelea kuwa mwaminifu kwa Chama Cha Mapinduzi (CCM) hadi atakapofariki dunia, huku akiwashukuru Spika Ndugai na Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, kwa kuwa walimu wazuri kwake kiuongozi.

**MSAIDIZI WAKE ALIA**

Baada ya kikao cha mchana cha Bunge kuahirishwa huku Dk. Mpango akiondoka kwa msafara maalum ulioandaliwa kwa ajili yake, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Mwanaidi Ali Khamis, alitoka ukumbini akiwa anabubujikwa na machozi.

Alipofuatwa na Nipashe, Mwanaidi alisema amejisikia uchungu kumkosa Dk. Mpango katika wizara hiyo, akisisitiza kuwa mzaliwa huyo wa Buhigwe mkoani Kigoma ni mwalimu mzuri wa uchumi.

***Imeandikwa na Sanula Athanas, DODOMA na Epson Luhwago, DAR.***

## Kutoka familia maskini hadi Ikulu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MIAKA mitano iliyopita, aliteuliwa kuwa Waziri wa Fedha akiwa mbunge wa kuteuliwa na jana Rais Samia Suluhu Hassan alimteua kuwa Makamu wa Rais na kupendekeza bungeni athibitishwe.

Jina lake halikuwa miongoni mwa majina ya makada wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) waliokuwa wanatajwa kwamba huenda mmojawapo angeteuliwa kushika nafasi ya Makamu wa Rais.

Baada ya jina lake kuwasilishwa bungeni jana na Mpambe wa Rais, lilikuwa lake na Spika wa Bunge, Job Ndugai, kuzungumza na wabunge waliokuwa na 'rungu'. Huyo si mwingine bali ni Dk. Philip Mpango.

Dk. Mpango, aliyezaliwa Wilaya ya Buhigwe mkoani Kigoma Julai 14, 1957 ametoka mbali mpaka kufikia hatua ya kushika wadhifa huo mkubwa katika serikali. Anajinasibu kuwa ametoka katika familia ya kimaskini na amevaa viatu wa umaskini.

Ni mtu aliyesoma seminari na wakati huo watu hao walikuwa wakionekana kuandaliwa kuwa mapadri lakini haikuwa hivyo.

Akijieleza mbele ya bunge jana, alisema upadri ulimshinda na kuamini kuwa Mungu hakumpangia wito huo.

Baada ya kumaliza kidato cha sita alijiunga na Jeshi la Kujenga Taifa kwa mujibu wa sheria katika kambi za Bulombora, Kigoma na baadaye JKT, Mlale, Songea. Baada ya hapo alifanya kazi lililokuwa Shirika la Akiba ya Wafanyakazi (NPF sasa NSSF) na katika nafasi ya Ofisa Uhusiano Msaidizi na baadaye Mtafiti Msaidizi katika Shirika la Ugavi la Elimu (TES).

"Nilikwenda UDSM, nilifanya Shahada ya Uchumi na nilihitimu shahada ya kwanza mwaka 1984, baada ya pale nilifanya kazi Wizara ya Kazi kwenye Idara ya Nguvu Kazi mwaka 1985 hadi 1986 niliporejea UDSM kwa shahada ya pili kwenye uchumi," alisema.

Mwaka 1988, alipohitimu shahada ya pili ya uchumi aliajiriwa kuwa Mhadhiri Msaidizi na mwaka uliofuata alianza shahada ya uzamivu Chuo Kikuu cha Lund, Sweden ambako kulikuwa na mafunzo na utafiti. Alihitimu mwaka na kuendelea kufanya kazi UDSM akiwa mhadhiri idara ya uchumi na utafiti.

"Mwaka 2002 nikaomba likizo nikaenda kufanya kazi Benki ya Dunia (WB) kama mchumi mwandamizi. Haukuwa uamuzi mwepesi sana, niliamua kwenda kule ili nijifunze taasisi kubwa hizi zinavyosukuma sera kwa nchi zetu, zinafanyaje kazi, kuna nini kule ndani?

"Niliaminiwa kusimamia baadhi ya miradi hasa upande wa matumizi ya serikali, nilikuwa katibu wa ile timu ya WB. Rais Jakaya Kikwete aliniteua kuwa msaidizi wake wa masuala ya uchumi kutoka WB. Nilianza kazi ile mpaka mwaka 2010 Rais Kikwete aliniteua kuwa Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na alinihamisha kuwa Mkuu wa Tume ya Mipango.

"Rais Magufuli aliniteua kutoka pale akanipeleka kuwa Kaimu Kamishna Mkuu wa TRA, nilifanya kazi kwa mshangao kama leo kwa muda wa takriban mwezi mmoja, ilikuwa kazi ngumu, tulipewa kazi ya lazima tuongeze mapato ya serikali.

"Wakati nikidhani nimezoea kukusanya mapato na changamoto zake, saa mbili usiku tarehe 23 nikiwa ofisini, rafiki zangu wakaniambia Rais ameniteua kuwa mbunge na Waziri wa Fedha na Mipango.

"Alipokufa Magufuli, nililia sana hadharani na binafsi nyumbani, lakini machozi yangu yalikauka kwa sababu lazima taifa letu liendelee kuongozwa na Watanzania na kazi yetu kubwa ni moja tu," alisema.



Makamu wa Rais mteule, Dk. Philip Mpango (kulia), akiaga rasmi bungeni jijini Dodoma jana, baada ya wabunge kupitisha jina lake kwa asilimia 100, ili kushika nafasi hiyo na kupoteza sifa ya kuwa mbunge. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Kitendawili kilivyoteguliwa

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

BAADA ya kuwapo tetesi za uwezekano wa makada wakongwe kadhaa wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) kuteuliwa kushika nafasi ya Makamu wa Rais wa Tanzania, hatimaye Rais Samia Suluhu Hassan amemteua Dk. Philip Mpango kushika wadhifa huo.

Uteuzi wa Dk. Mpango, ambaye awali alikuwa Waziri wa Fedha na Mipango, umefanyika zikiwa zimebaki siku tatu kabla ya kukamilika kwa muda wa kikatiba wa siku 14 zinazomtaka Rais kuteua Makamu wa Rais.

Bahasha yenye jina la mteule iliwasilishwa bungeni jana asubuhi na mpambe wa Rais na kuibua shangwe kwenye chombo hicho cha kutunga sheria.

Baada ya kumalizika kwa kipindi cha 'Maswali na Majibu' bungeni asubuhi, Spika Job Ndugai aliingia bungeni kuongoza shughuli za Bunge akipishwa kwenye kiti na Naibu Spika, Dk. Tulia Ackson, aliyeongoza shughuli za awali.

Spika Ndugai aliagiza askari wa usalama bungeni wamwingize bungeni mgeni maalum, Mpambe wa Rais, Kanali Nyamburi Mashauri, aliyekuwa na ujumbe mahususi kutoka kwa Rais Samia. Baada ya kuingia bungeni, Mpambe wa Rais alikwenda moja kwa moja hadi kwa Spika na kumkabidhi bahasha ambayo ilikuwa na barua kutoka kwa Rais.

Spika baada ya kupokea ujumbe huo, huku akimsifu aliyeuwasilisha kwa kuwa mwanamke wa kwanza nchini kuwa Mpambe wa Rais, aliwasomea wabunge kilichoandikwa akianika kuwa Rais amempendekeza Dk. Mpango kuwa Makamu wa Rais.

"Mheshimiwa Rais kwa mamlaka aliyopewa na Katiba chini ya Ibara ya 37(5), amempendekeza afuataye kuwa Makamu wa Rais wa Tanzania. Aliyependekezwa... (akasita) Nitasoma karatasi hii kama ilivyo.

"Kwa hiyo ninakuu, imeandikwa hivi: "Mheshimiwa Spika, ninawasilisha bungeni jina la Mheshimiwa.... (akasita). Ninarudia tena... Makatibu ninaomba maji ya kunywa... (kukawa na kicheko kwa muda).

"Jamani mko tayari eeh! Mheshimiwa Rais anasema 'Mheshimiwa Spika, ninawasilisha bungeni jina la Dk. Philip Mpango kwa nafasi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania'," Spika Ndugai alisema na kuibua shangwe bungeni.

Baada ya kutangazwa kwa jina hilo, baadhi ya mawaziri, wakiwamo Dk. Medard Kalemani (Nishati), William Lukuvi (Ardhi) na Jenista Mhagama (Ofisi ya Waziri Mkuu) waliinuka kwenye viti vyao na kumfuata kumpongeza Dk. Mpango aliyekuwa ameketi huku akionekana kupigwa butwaa akikutanisha viganja vya mikono yake kwa ishara ya mtu anayeshukuru.

Wakati utaratibu wa Bunge kupiga kura kupitisha jina hilo ukiandaliwa, Spika Ndugai alimpa nafasi Dk. Mpango kuzungumza na wabunge kwa dakika chache. Muda wote huo, Dk. Mpango alikuwa ameketi kwenye kiti chake cha Waziri wa Fedha na Mipango.

Baadaye, Ndugai alitoa nafasi kwa wabunge wachache kumzungumzia Dk. Mpango. Waliopewa nafasi hiyo ni pamoja na Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Profesa Joyce Ndalichako, aliyemsifu mtaalamu huyo wa uchumi kwa kile alichodai kuwa ana uchungu na nchi.

Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Lukuvi, alisema Dk. Mpango ana uwezo mkubwa wa kufanya kazi na anamtanguliza Mungu katika mambo yake.

"Dk. Mpango ni mcha Mungu sana. Mtembelee nyumbani kwake Chanika, ukifika huko, nyumba yake tu inaonyesha kwamba huyu ni mcha Mungu. Hata alipopata matatizo hivi karibuni, alimtanguliza Mungu sana," alisema.

Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Profesa Palamagamba Kabudi, alisema kuwasilishwa kwa jina la Dk. Mpango bungeni kupitishwa kuwa Makamu wa Rais, ni majibu ya maombi ya mama yake kwa Mungu, akibainisha kuwa Dk. Mpango alimpoteza baba yake akiwa kwenye umri mdogo.

Mbunge wa Kawe, Josephat Gwajima, alimpongeza Rais Samia, kwa kumpendekeza Dk. Mpango kushika nafasi hiyo, akisema "jicho lililomwona Dk. Mpango ni kubwa kuliko aliyeteuliwa".

Mbunge wa Geita, Joseph Musukuma, alimpongeza Rais Samia kwa kuwasilisha jina la Dk. Mpango ambaye alimsifia kwa kile alichodai hana makundi na anamsikiliza kila mtu.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), Naghenjwa Kaboyoka, alisema Dk. Mpango ni mnyenyekevu hata kwenye mambo magumu, akibainisha kuwa alimpa ushirikiano mkubwa alipomfuata kumtaka atoe ufafanuzi kuhusu sakata la kudaiwa kutoonekana kwa Sh. trilioni 1.5 katika matumizi ya serikali miaka mwili iliyopita.

"Nilipomfuata kupata ufafanuzi kuhusu sakata la Sh. trilioni 1.5, Dk. Mpango alinieleza ukweli kwamba 'kuna matatizo ya mfumo na tunayarekebisha. Mimi sikujua kwamba ni yatima," alisema.

Baada ya wabunge kupiga kura, Spika Ndugai alitangaza kuwa Dk. Mpango amepitishwa na wabunge wote 363 waliokuwapo bungeni jana na kupiga kura za 'NDIYO'.

Spika wa Bunge, Job Ndugai, baada ya Bunge kupiga kura kuthibitisha uteuzi wa Rais kwa nafasi hiyo, alitangaza kwamba kwamba Jimbo la Buhigwe mkoani Kigoma sasa liko wazi kutokana na Dk. Mpango kuteuliwa kushika nafasi hiyo.

## Wadau wasema 'viatu' vinamtosha

**Na Christina Mwakangale**

MASHIRIKA na baadhi ya wananchi wakiwamo wanasiasa wamepongeza uteuzi wa Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, kushika nafasi hiyo kutokana na uzoefu wake wa kuwa mchumi mbobevu na mataalam wa masuala ya fedha.

Mkurugenzi wa Jukwaa la Katiba (JUKATA), Chacha Wangwe, alisema ni chaguo sahihi kwa kuwa suala la uchumi analichukulia kwa ukubwa jambo ambalo linaonyesha kuwa atakuwa msaidizi mzuri wa Rais Samia.

"Rais Samia anataka kubadili mazingira ya viongozi waliolalamikiwa hasa siasa zilizopingwa kukandamiza demokrasia na uhuru wa habari."

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Anna Henga, alisema hawana mashaka na uwezo wa Dk. Mpango kwa kuwa ni mtu anayefahamu uchumi na anaelewa miradi ya maendeleo ambayo alikuwa anaisimamia.

"Tunaamini atamsaidia na kumshauri Rais Samia Suluhu Hassan, tunajua siyo mtu wa siasa nyingi hivyo atamshauri. Kwenye haki za binadamu hatuna shida na Rais na Makamu wake, tunaomba wajue asasi zinachangia uchumi wa nchi kwa kulipa kodi kutokana na fedha za miradi mbalimbali, nasi tutasaidiana kuhakikisha uchumi wetu unakua," alisema.

Aliwashauri watumishi na wananchi kwa kumuunga mkono Rais na Makamu wa Rais ili kufikia maendeleo yanayotakiwa.

Naye Mchumi Prof. Godius Kakyarara, alisema anaiona awamu ya uchumi kutokana na ukweli Rais Samia ana taaluma ya uchumi pamoja na Makamu wake ambayo itasaidia kulisogeza taifa.

"Dk. Mpango amekuwa katika awamu zote za Mpango wa Maendeleo kwa hiyo masuala ya maendeleo ya nchi anayajua, anaweza kufanya kazi nzuri, huyu ni chaguo sahihi kwa Tanzania," alisema.

Mwanasiasa Athony Komu, alisema uteuzi wa Dk. Mpango, unafaa ingawa kuna baadhi ya masuala ya kufanyiwa kazi.

"Elimu yake inatosha ingawa alikuwa mchumi, alifanya Tume ya Mipango, Wizara ya Fedha hapo shida naiona katika chama chake."



Mkurugenzi wa Taasisi ya Al-Hikma, Nurdin Kishik (kulia), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu maandalizi ya mashindano ya Quran, yakatayoshirikisha nchi 21 za Afrika na kufanyika kwenye Uwanja wa Mkapa, Aprili 25, mwaka huu. Kushoto ni Mjumbe wa Kamati Kuu ya Mashindano hayo, Zaki Ahmed. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Uchunguzi tuhuma ubadhirifu bandari mbioni kukamilika

**Na Romana Mallya**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), imesema iko katika hatua ya mwisho ya uchunguzi dhidi ya ubadhirifu wa fedha Sh. bilioni 3.6 uliofanywa kwenye Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA).

Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi hiyo, Brigedia Jenerali John Mbungo, alisema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumzia kuhusu kushikiliwa kwa Mkurugenzi Mkuu wa TPA, Mhandisi Deusdedit Kakoko, na kukanusha taarifa za fedha dola za Marekani milioni 1.6 ambazo zimesambaa mtandaoni zikidaiwa kukutwa nyumbani kwake.

Jenerali Mbungo alisema baada ya maagizo ya Rais Samia Suluhu Hassan, aliyotoa kwao, mara moja walianza utekelezaji na kumshikilia ili kufanya uchunguzi dhidi yake.

"TAKUKURU ipo imara na uchunguzi upo katika hatua za mwisho kukamilika ili hatua zingine za kisheria zichukuliwe dhidi ya watuhumiwa wote waliojihusisha na ubadhirifu wa fedha na matumizi mabaya ya fedha za serikali," alisema.

Kuhusu fedha zilizodaiwa kukutwa nyumbani kwa Mhandisi Kakoko, Mbungo alisema siyo za kweli na kufafanua kuwa fedha zilizokutwa baada ya upekuzi ni Dola za Marekani 3,000 na Sh. milioni 1.5.

"Zipo taarifa zinazosambaa mtandaoni zikidai kwamba TAKUKURU ilipokwenda nyumbani kwake kufanya upekuzi ilikuta kiasi kikubwa cha fedha Dola za Marekani milioni 1.6.

"Ninakanusha taarifa hizi, hazina ukweli wowote, TAKUKURU katika upekuzi walikuta kiasi kidogo sana cha fedha, Dola za Marekani 3000 na Sh. milioni 1.5, ningependa wananchi wafahamu kwamba taarifa hizi zinazozagaa, zinaonyeshwa mitandao mbalimbali si za kweli," alisema.

Alisema upekuzi ulizingatia matakwa yote ya kisheria na walimshirikisha kiongozi wa Serikali ya Mtaa na baadhi ya wanafamilia wa Kakoko na wachunguzi walishuhudia namna ulivyofanyika.

Aliwaomba wananchi wapuuzie taarifa hizo zilizozagaa mtandaoni na waamini kwamba TAKUKURU inafanya uchunguzi ambao tayari ulishaanza tangu Machi, mwaka jana.

Jumapili, wakati akipokea ripoti ya TAKUKURU na ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali (CAG) ya mwaka 2019/20, Rais Samia aliagiza kusimamishwa kazi, Mhandisi Kakoko ili kupisha uchunguzi wa ubadhirifu wa fedha hizo uliofanyika bandarini hapo. Rais Samia alisema ripoti aliyokabidhiwa inaonyesha kuna ubadhirifu wa Sh. bilioni 3.6, karibu bilioni nne.

"Lakini, wakati Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, amefanya ukaguzi waliosimamishwa ni hawa wa chini, naomba mara moja nitoe agizo la kumsimamisha Mkurugenzi Mkuu wa Bandari, halafu uchunguzi uendelee," alisema.

## Sita wafariki dunia katika ajali ya basi

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

WATU sita wamefariki dunia papo hapo katika ajali ya gari la Machame Investment lenye namba za usajili T.479 DRF linalofanya safari kati ya Dodoma na Arusha.

Akizungumza katika eneo la Kiongozi ajali ilikotokea, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Manyara, Paul Kasabago, alithibitisha kutokea kwa ajali hiyo na kwamba waliofariki dunia wanne ni wanaume akiwamo dereva na wawili ni wanawake.

Kasabago alisema ajali hiyo ilitokea majira ya saa 8:00 mchana na chanzo cha ajali hiyo ni utelezi kwa kuwa mvua ilikuwa inanyesha.

Pia alisema idadi kubwa ya abiria waliokuwa kwenye gari hilo walikuwa wanafunzi ambao walikuwa wanaenda likizo ya Pasaka.

Kamanda huyo alisema idadi ya majeruhi bado haijajulikana kwa kuwa wakati akizungumza ilikuwa muda mfupi baada ya ajali na kwamba wamepelekwa Hospitali ya Mji wa Babati Mrara.

Katika hatua nyingine. sintofahamu imetanda katika eneo la Weruweru, Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro kuhusu kisa cha baba wa familia moja kuwapiga risasi mkewe na mwanawe wa kiume, anaripoti GODFREY MUSHI kutoka Moshi.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kilimanjaro, Kamishna Msaidizi (ACP), Amon Kakwale, alisema jana kuwa chanzo cha tukio hilo bado hakijafahamika.

"Majeruhi waliopigwa risasi wanapatiwa matibabu katika Hospitali ya Rufani ya Kanda ya KCMC na hali zao bado si nzuri.

"Hata hivyo, mtuhumiwa aliyetekeleza unyama huo tunamshikilia pamoja na bastola anayoimiliki kihalali," alisema Kamanda.

Anayeshikiliwa na Jeshi la Polisi kwa tuhuma hizo ni Alison Albert (61), mkazi wa Weruweru wilayani Hai.

Mtuhumiwa huyo anadaiwa kumpiga risasi kifuani na tumboni mke wake Magreth Albert (51) pamoja na mwanawe wa kiume Albert Alison (28), anayedaiwa kupigwa risasi mgongoni.

Ofisa Uhusiano wa Hospitali ya Rufani ya KCMC, Gabriel Chisseo, alipofuatwa kuthibitisha kama majeruhi wa tukio hilo, alikiri kuwa walipokewa hospitalini hapo.

"Ni kweli tuliwapokea jana jioni (juzi) na mama bado hali yake si nzuri amelazwa katika chumba cha uangalizi maalum (ICU) akipatiwa matibabu. "Lakini majeruhi Albert yeye anaendelea vizuri, tunaona kama afya yake inaimarika, yuko wodini."


bgtl BEST GROUP (T) LIMITED
Debts collectors, Auctioneer, Commission Agent & Legal Consultant

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

Kwa Idhini tuliyopewa na **BANC ABC** Tunatoa notisi ya siku kumi na nne (14) kuanzia Tarehe ya Tangazo hili kwa mdaiwa aliyetajwa hapo chini, alipe deni analodaiwa na benki hiyo pamoja na riba. Kushindwa kulipa kwa muda huo tutalazimika kuuza dhamana (mali) iliyodhamini mkopo wake kwa **MNADA WA HADHARA.** Mnada utafanyika kuanzia saa 4:00 Asubuhi na kuendelea mahali dhamana ilipo kama inavyoonesha hapo chini.

| Na. | JINA LA MDAIWA | MAELEZO YA DHAMANA NA MAHALI ILIPO |
|---|---|---|
| 1. | **ABDUL SAMAD HASSAN T/A PAULA INTERBUSINESS CO.LTD** | Nyumba ya makazi iliyopo kwenye kiwanja na.1178 yenye Hati na.80179 Kitalu "F" ofisi ya Ardhi na.283031 eneo la Magogoni jijini Dar es Salaam. |

**MASHART YA MNADA**
1. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
2.Mnunuzi atatakiwa kulipa siku ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3 .Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14). Kukamilisha malipo yote. Kushindwa kufanya hiyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25%, na mnada kurudiwa, au mshindi wa pili atapewa ushindi.
4. Gharama za kuona, kukagua, kuhamisha umiliki, kumtoa mdaiwa/mpangaji na zingine zinazoambatana na hilo ni jukumu la mnunuzi.

**Kwa Taarifa zaidi wasiliana na:** **AU**
**Mkurugenzi Mtendaji**
**Best Group (T) LTD**
**Alli Hassan Mwinyi Road.**
**Green Acres Building, 2nd Floor.**
**P.O. BOX 1088**
**Dar Es Salaam**
**Mob: + 255 715-363537/ +255 765-363537**

**Mkurugenzi Mtendaji**
**Banc ABC**
**Head Office,**
**Uhuru Heights,5th &6th Floor, Bibi Titi Mohamed**
**P.O. BOX 31,**
**Dar Es Salaam, Tanzania**
**Tel: +255-22-2119422-3**
**Web: www.bancabc.co.tz**



bgtl BEST GROUP (T) LIMITED
Debts collectors, Auctioneer, Commission Agent & Legal Consultant

**TANGAZO LA MNADA WA HADHARA**

Kwa Idhini tuliyopewa na **BANK OF AFRICA** Tunatoa notisi ya siku kumi na nne(14) kuanzia Tarehe ya Tangazo hili kwa mdaiwa aliyetajwa hapo chini, alipe deni analodaiwa na benki hiyo pamoja na riba. Kushindwa kulipa kwa muda huo tutalazimika kuuza dhamana (mali) iliyodhamini mkopo wake kwa **MNADA WA HADHARA.** Mnada utafanyika kuanzia saa 4:00 Asubuhi na kuendelea mahali dhamana ilipo kama inavyoonesha hapo chini.

| Na. | JINA LA MDAIWA | MAELEZO YA DHAMANA NA MAHALI ILIPO |
|---|---|---|
| 1. | **GOZA FOOD AND PACKAGING (T) LTD/ GODFREY ZACHARIA NSERERE** | Nyumba ya Biashara yenye leseni ya makazi Na.KND 026731 chini ya kifungu Na. KND/TND/FKC11/78 eneo la Pakacha,Tandale Manispaa ya Kinondoni . |

**MASHART YA MNADA**
1. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa siku ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14). Kukamilisha malipo yote. Kushindwa kufanya hivyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25%, na mnada kurudiwa, au mshindi wa pili atapewa ushindi.
4. Gharama za kuona, kukagua, kuhamisha umiliki, kumtoa mdaiwa/mpangaji na zingine zinazoambatana na hilo ni jukumu la mnunuzi.

**Kwa Taarifa zaidi wasiliana na:** **AU**
**Mkurugenzi Mtendaji**
**Best Group (T) Ltd**
**Alli Hassan Mwinyi Road**
**Green Acres Buliding, 2nd Floor**
**P.O. BOX 1088**
**Dar Es Salaam.**
**Mob: + 255 715-363537/ +255 765-363537**

**Mkurugenzi Mtendaji**
**Bank of Africa**
**Head Office,**
**NDC Development House, Ohio street/kivukoni**
**P.O. BOX 3054,**
**Dar Es Salaam, Tanzania.**
**el: +255-22-2110104/2111290**
**Fax: +255-22-2113740**

**HABARI KITAIFA**

# Usajili wa VICOBA sasa waanza rasmi

**Na Salome Kitomari**

BENKI Kuu ya Tanzania (BoT), imesema usajili wa vikundi vya kijamii vya huduma ndogo za fedha, umeanza na kuwataka wenye vikundi vya VICOBA kujisajili kabla ya Aprili 30, mwaka huu.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Idara ya Uhusiano wa Umma na Itifaki ya BoT, vikundi vinatakiwa kuwasilisha maombi ya usajili katika halmashauri husika ili yafanyiwe kazi na mamlaka husika.

"Aprili 30, mwaka huu, ndio mwisho wa kupokea maombi ya usajili kwa vikundi vya kijamii vya huduma ndogo za kifedha vilivyokuwa vikifanya shughuli zake.

"Kikundi kitapata changamoto kufanya usajili kwa njia ya kielektroniki, inashauriwa kipeleke maombi hayo kwa Ofisa Maendeleo ya Jamii aliyeko katika ofisi ya kata au halmashauri iliyo karibu kwa ajili ya msaada zaidi," ilifafanua taarifa hiyo.

BoT ilisema kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) inaviarifu vikundi (VICOBA) kuhakikisha kuwa vinawasilisha maombi ya usajili kwenye mamlaka za serikali za mitaa husika kabla ya Aprili 30, mwaka huu.

Aidha, BoT imevionya vikundi vitakavyoendelea kufanya biashara ya huduma ndogo za fedha bila kusajiliwa vitakuwa vinavunja sheria na hatua kali zitachukuliwa na kwamba vinaweza kujisajili kupitia https://cmg.go.tz/cmg-portal/login.

"Usajili wa vikundi vya kijamii vya huduma ndogo za fedha ni utekelezaji wa Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha ya 2018 inayolenga kuhakikisha kuwa sekta ya huduma ndogo za fedha inasimamiwa vizuri ili kuwa imara na kuchangia juhudi za serikali za kuongeza upatikanaji wa huduma za fedha na kupunguza kiwango cha umaskini katika jamii ya Watanzania," ilifafanua taarifa hiyo.

Pia taarifa hiyo ilisema BoT iko tayari kutoa msaada utakaohitajiwa na kikundi chochote na imeandaa mfumo wa kieletroniki wa usajili wa vikundi vya kijamii vya huduma ndogo za fedha kwa kushirikiana na TAMISEMI.

Mfumo huu wa kielektroniki, taarifa ilisema unalenga kuviwezesha vikundi vyote vya kijamii vya huduma ndogo za fedha kuwasilisha maombi ya usajili kwa njia ya kielektroniki.

# Wataalamu TEHAMA kujadili ripoti ya CAG

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Dk. Faustine Ndugulile, ameagiza kuitishwa leo kwa kikao cha wataalamu wa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), ili kuzishughulikia hoja za ukaguzi zilizobainishwa na Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali (CAG).

Katika taarifa ya CAG, ilionesha masuala ya mifumo ya TEHAMA ndani ya serikali haisomani, haizungumzi na haiingiliani.

Akizungumza jana na waandishi wa habari, Dk. Ndugulile alimtaka Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Dk. Zainabu Chaula, kuratibu kikao cha Makatibu Wakuu wa Wizara zinazohusika na mifumo ya TEHAMA pamoja na kuitisha kikao cha wakurugenzi wanaosimamia TEHAMA wa wizara na taasisi za serikali ili kujadili matatizo yaliyojitokeza na kushauri namna ya kuzitatua.

"Wizara imechukua kwa uzito unaostahili hoja za ukaguzi za CAG zinazohusu kero za baadhi ya mifumo ya TEHAMA kama zilivyoelekezwa na CAG wakati akiwasilisha taarifa yake kwa Rais Samia Suluhu Hassan Machi 28, mwaka huu," alisema.

Dk. Ndugulile alimwagiza kuitishwa kwa kikao hicho leo ili kupata ushauri wa kitaalamu wa kushughulikia kero hizo.

Alizitaja wizara na taasisi zitakazohusika kwenye kikao hicho ni Ofisi ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Wizara ya Fedha na Mipango, CAG, Mamlaka ya Mawasilliano Tanzania na Shirika la Mawasiliano Tanzania.

Nyingine ni Kituo cha Taifa cha Kuhifadhi Data, Mamlaka ya Mapato Nchini (TRA) na Mamlaka ya Serikali Mtandao kujadili na kupata majibu ya hoja hizo.

Kadhalika, Dk. Ndugulile alisema TEHAMA inatumika kutoa huduma za mtandao za serikali kwa wananchi katika sekta ya afya, elimu, fedha, kilimo, biashara pamoja na serikali mtandao.

Hata hivyo, alisema pamoja na mafanikio hayo na matumizi mazuri ya mifumo hiyo, bado kumekuwapo na matatizo ya utengenezaji, uendeshaji na uendelezaji wa mifumo ya TEHAMA.

Alisema matatizo hayo ni mifumo kutounganishwa au kutobadilishana taarifa na utegemezi wa wataalamu wa taasisi nyingine kwenye kujenga na kuendesha mifumo.

Nyingine ni uwapo wa mifumo yenye kazi zinazofanana na baadhi yake haifanyi kazi kwa ufanisi kama ilivyokusudiwa.

Alitaka kazi hiyo ifanyike na kukamilika mapema ndani ya wiki moja ili kuipata na kushauri serikali na mamlaka namna bora ya kutengeneza, kuendesha na kuendeleza mifumo ya TEHAMA nchini.

Akizungumzia kuhusu siku 100 baada ya kuundwa kwa wizara hiyo, Waziri Ndugulile alisema kumekuwa na ongezeko la miamala ya fedha inayopita mtandaoni kwa mwezi kutoka wastani wa Sh. milioni 310 kwa Desemba 2020 mpaka Sh. milioni 340 hadi Machi 5, mwaka huu.

Alisema pia wastani wa Sh. trilioni 20 zimepita mtandaoni kati ya Desemba 2020 hadi Machi, mwaka huu ikilinganishwa na wastani wa Sh. trilioni 18 kwa mwezi katika kipindi cha Desemba 5, mwaka huu.


**Canara Bank (Tanzania) Ltd.**

(Together, we can build a better life)

## UONESHAJI WA TAARIFA ZA FEDHA ZILIZOKAGULIWA KWA UMMA

**Imetolewa chini ya kanuni ya 7 na ya 8 ya Kanuni za Mabenki na Taasisi za Fedha (Uoneshaji) ya Mwaka 2014**

### WARAKA WA MIZANIA ULIOKAGULIWA KWA TAREHE 31 DESEMBA 2020

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | | Mwaka wa Sasa 31 Desemba 2020 | Mwaka wa Uliopita 31 Desemba 2019 |
|---|---|---|---|
| A | **ASSETS** | | |
| | 1 Fedha Taslimu | 1,279.03 | 405.33 |
| | 2 Salio katika Benki kuu ya Tanzania | 3,824.46 | 6,601.31 |
| | 3 Uwekezaji katika Amana za serikali | 30,890.00 | 25,371.80 |
| | 4 Salio katika Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 621.27 | 668.44 |
| | 5 Hundi na Miamala ya Kushughulikiwa | 32.00 | 67.32 |
| | 6 Miamala Baina ya Matawi | 0.00 | 0.00 |
| | 7 Bili zilizoafikiwa | 0.00 | 0.00 |
| | 8 Dhima za Wateja Zilizokubalika | 0.00 | 0.00 |
| | 9 Mikopo Iliyotolewa kwa Benki Nyingine | 34,455.39 | 36,866.46 |
| | 10 Uwekezaji Katika Amana Nyingine | 0.00 | 0.00 |
| | 11 Mikopo Halisi Iliyopo | 48,424.85 | 35,634.01 |
| | 12 Mali Nyingine | 917.50 | 838.23 |
| | 13 Uwekezaji wa Hisa | 0.00 | 0.00 |
| | 14 Akaunti za udhamini | 0.00 | 0.00 |
| | 15 Mali Zisizohamishika, Mitambo na Vifaa | 1,123.04 | 1,556.18 |
| | **16 JUMLA YA MALI** | **121,567.55** | **108,009.07** |
| B | **DHIMA** | | |
| | 17 Amana za Benki nyingine na Taasisi za Fedha | 33,084.50 | 32,500.00 |
| | 18 Amana za Wateja | 48,164.40 | 37,399.46 |
| | 19 Dhamana ya Malipo kwa Fedha Taslimu | 0.00 | 0.00 |
| | 20 Amana Maalumu | 0.00 | 0.00 |
| | 21 Maagizo ya Malipo/Fedha za Kuhamisha | 0.00 | 0.00 |
| | 22 Hundi na Hawala za Kibenki Zilizotolewa | 0.00 | 0.00 |
| | 23 Limbiko la Kodi na Gharama Zitakazolipwa | 2,064.56 | 1,302.99 |
| | 24 Dhima la Tozo kwa Ajili ya Usuluhishi Baina ya Benki na Mteja | 0.00 | 0.00 |
| | 25 Miamala Isiyoshughulikiwa Baina ya Matawi | 0.00 | 0.00 |
| | 26 Mapato yaliyoingia ya Kipindi Kijacho na Tozo Nyingine Zitakazolipwa Baadae | 0.00 | 0.00 |
| | 27 Dhima Nyingine | 628.52 | 839.34 |
| | 28 Madeni | 0.00 | 0.00 |
| | **29 JUMLA YA DHIMA** | **83,941.98** | **72,041.79** |
| | **30 MALI/(DHIMA) HALISI** *(16 kutoa 29* | **37,625.57** | **35,967.28** |
| C | **FEDHA ZA WANAHISA** | | |
| | 31 Mtaji wa Hisa Uliolipwa | 32,830.00 | 32,830.00 |
| | 32 Akiba ya Mtaji | 41.35 | 828.58 |
| | 33 Mapato Yaliyobakizwa | 3,095.93 | 836.39 |
| | 34 Faida (Hasara) ya Kipindi Husika | 1,658.29 | 1,472.31 |
| | 35 Akaunti Nyingine za Mtaji | 0.00 | 0.00 |
| | 36 Stahiki ya Wenyehisa Chache | 0.00 | 0.00 |
| | **37 JUMLA YA FEDHA ZA WANAHISA** | **37,625.57** | **35,967.28** |
| | 38 Dhima Zisizo Dhahiri | 10,219.56 | 10,781.42 |
| | 39 Mikopo Chechefu | 1,319.31 | 4,125.84 |
| | 40 Tengo kwa Ajili ya Mikopo Chechefu | 364.15 | 162.90 |
| | 41 Mali Nyingine Chechefu | 0.00 | 0.00 |
| D | **BAADHI YA VIASHIRIO VYA HALI YA KIFEDHA** | | |
| | (i) Uwiano wa Fedha za Wanahisa na Jumla ya Mali | 30.95% | 33.30% |
| | (ii) Uwiano wa Mikopo Chechefu na Jumla ya Mikopo Ghafi | 2.71% | 11.49% |
| | (iii) Uwiano wa Mikopo Ghafi na Jumla ya Amana | 60.03% | 51.14% |
| | (iv) Uwiano wa Mikopo Halisi na Jumla ya Mali Halisi | 39.83% | 33.24% |
| | (v) Uwiano wa Mali Zinazozalisha na Jumla ya Mali | 94.10% | 91.23% |
| | (vi) Ongezeko la Amana | 16.24% | 5.01% |
| | (vii) Ongezeko la Mali | 12.55% | 5.60% |

### TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI ILIYOKAGULIWA KWA MWAKA UNAOISHIA TAREHE 31 DESEMBA 2020

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | Mwaka wa Sasa 31 Desemba 2020 | Mwaka wa Uliopita 31 Desemba 2019 |
|---|---|---|
| 1 Mapato ya Riba | 8,750.58 | 8,167.40 |
| 2 Gharama za Riba | 3,292.98 | 2,802.03 |
| **3 Mapato Halisi ya Riba (1kutoa 2)** | **5,457.60** | **5,365.37** |
| 4 Madeni Viza Yaliyofutwa | 0.00 | 0.00 |
| 5 Punguzo/Ongezeko la tengo katika Mikopo | 201.25 | 61.62 |
| **6 Mapato Yasiyo ya Riba** | **850.83** | **825.55** |
| 6.1 Faida /(Hasara) Zitokanazo na Miamala ya Fedha za Kigeni | 174.73 | 137.86 |
| 6.2 Ada na Kamisheni | 676.10 | 687.70 |
| 6.3 Gawio | 0.00 | 0.00 |
| 6.4 Mapato Mengine | 0.00 | 0.00 |
| **7 Gharama Zisizo za Riba:** | **3,524.73** | **3,978.19** |
| 7.1 Mishahara na Mafao | 1,295.53 | 1,447.60 |
| 7.2 Ada na Kamisheni | 30.77 | 0.00 |
| 7.3 Gharama Nyingine | 2,198.43 | 2,530.59 |
| **8 Faida /(Hasara) ya Uendeshaji** | **2,582.45** | **2,151.12** |
| 9 Tengo la Kodi ya Mapato | 924.16 | 678.81 |
| **10 Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato** | **1,658.29** | **1,472.31** |
| 11 Idadi ya Waajiriwa | 25 | 25 |
| 12 Mapato kwa Hisa | 51 | 45 |
| 13 Mapato kwa Hisa | 51 | 45 |
| **14 Idadi ya Matawi** | 1 | 1 |
| **BAADHI YA VIASHIRIO VYA UFANISI** | | |
| (I) Uwiano wa Faida Kabla ya Kodi na Wastani wa Mali | 1.46% | 1.40% |
| (II) Uwiano wa Faida baada ya Kodi na Wastani wa Fedha za Wanahisa | 4.49% | 4.18% |
| (III) Uwiano wa Matumizi Yasiyo ya Riba na Mapato Ghafi | 55.87% | 64.26% |
| (IV) Uwiano wa Mapato Halisi ya Riba na Wastani wa Mali Zinazozalisha | 5.27% | 5.56% |

### TAARIFA YA MTIRIRIKO WA FEDHA ULIOKAGULIWA KWA MWAKA UNAOISHIA 31 Desemba 2020

*(Kiasi kwa shilingi milioni)*

| | | Mwaka wa Sasa 31 Desemba 2020 | Mwaka wa Uliopita 31 Desemba 2019 |
|---|---|---|---|
| I | **Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za uendeshaji:** | | |
| | Mapato/(Hasara) Halisi | 1,658.29 | 1,472.31 |
| | Marekebisho kwa ajili ya: | 0.00 | 0.00 |
| | Hasara katika mali | 894.96 | 1,300.77 |
| | -Badiliko halisi katika Mikopo | (14,001.25) | (842.93) |
| | Faida/Hasara kwenye mauzo ya Mali | 0.00 | 0.00 |
| | Mabadiliko halisi katika Amana | 11,349.44 | 3,336.53 |
| | Mabadiliko halisi katika Amana za muda Mfupi Zilizoafikiwa | 0.00 | 0.00 |
| | Mabadiliko halisi katika dhima nyingine | 1,671.43 | 794.93 |
| | Mabadiliko Halisi katika mali nyingine | (189.86) | (931.66) |
| | Kodi iliyolipwa | (891.19) | (612.79) |
| | Mengineyo(bainisha) | 0.00 | 0.00 |
| | **Fedha halisi zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za uendeshaji** | **491.82** | **4,517.15** |
| II | **Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za uwekezaji:** | | |
| | Gawio lililopokewa | 0.00 | 0.00 |
| | Ununuzi wa Mali za kudumu | (58.41) | (19.39) |
| | Mapato kutokana na mauzo ya mali za kudumu | 0.00 | 0.00 |
| | Ununuzi wa Amana zilizoshughulikiwa na Mawakala | (11,676.21) | 978.16 |
| | Mapato kutokana na mauzo ya Amana zilizoshugulikiwa na Mawakala | 0.00 | 0.00 |
| | Mengineyo(bainisha) | 0.00 | 0.00 |
| | **Fedha halisi zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za uwekezaji** | **(11,734.62)** | **958.77** |
| III | **Mtiririko wa fedha kutokana na shughuli za kifedha:** | | |
| | Ulipaji wa Madeni ya Muda Mrefu | 0.00 | 0.00 |
| | Mapato kutokana na Utoaji wa Madeni ya Muda Mrefu | 0.00 | 0.00 |
| | Mapato kutokana na utoaji wa Mtaji wa Hisa | 0.00 | 0.00 |
| | Gawio Lililolipwa kwa Fedha taslimu | 0.00 | 0.00 |
| | Mabadiliko halisi katika Madeni Mengine | 0.00 | 0.00 |
| | Mengineyo(Malipo ya dhima kukodishwa)-IFRS 16 | (230.25) | (346.31) |
| | **Fedha Halisi Zilizotolewa(zilizotumika) kwa shughuli za kifedha** | **(230.25)** | **(346.31)** |
| IV | **Fedha Taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha taslimu** | | |
| | Ongezeko/Punguzo Halisi Katika Fedha taslimu na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu | **(11,473.04)** | **5,129.61** |
| | Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwanzoni mwa mwaka | 48,369.87 | 43,240.26 |
| | **Fedha na Mali Zinazofanana na Fedha Taslimu Mwishoni mwa mwaka** | **36,896.83** | **48,369.87** |

### TAARIFA YA MABADILIKO YA MTAJI ILIYOKAGULIWA KWA KIPINDI KINACHOISHIA 31 DESEMBA 2020

| | Mtaji wa Hisa | Malipo juu ya bei ya hisa | Mapato Yaliyobakizwa | Ziada ya kisheria | Tengo la Ziada ya jumla | Mengineyo (Bainisha) | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Mwaka wa sasa 2020** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | 32,830.00 | - | 2,308.69 | 828.58 | - | - | **35,967.28** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 1,658.29 | - | - | - | **1,658.29** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | 787.23 | (787.23) | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | - | - | - | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **32,830.00** | - | **4,754.21** | **41.35** | - | - | **37,625.56** |
| **Mwaka Uliopita 2019** | | | | | | | |
| **Salio la mwanzo wa mwaka** | 32,830.00 | - | 1,125.67 | 45.93 | 493.37 | - | **34,494.97** |
| Faida / (Hasara) Halisi Baada ya Kodi ya Mapato | - | - | 1,472.31 | - | - | - | **1,472.31** |
| Mapato mengine yaliyojumuishwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Miamala na wanahisa | - | - | - | - | - | - | - |
| Gawio lililolipwa | - | - | - | - | - | - | - |
| Ziada ya Kisheria | - | - | (782.65) | 782.65 | - | - | - |
| Tengo la Ziada ya Jumla | - | - | 493.37 | - | (493.37) | - | - |
| Mengineyo | - | - | - | - | - | - | - |
| **Salio la mwisho wa mwaka** | **32,830.00** | - | **2,308.69** | **828.58** | - | - | **35,967.28** |

BAADHI YA MAELEZO
KWA MWAKA UNAOISHIA 31 DESEMBA 2020

Katika kuandaa taarifa za hizi za fedha,sera za uandaaji ni zilezile zilizotumika wakati wa uandaaji wa Taarifa za Fedha zilizokaguliwa za mwaka uliopita(kama kulikua na mabadiliko katika sera za uandaaji taarifa za fedha katika kipindi cha mwaka wa sasa,mabadiliko yaelezwe kwa mujibu wa IAS 34 na IAS 8)

| *Jina* | *Cheo* | *Sahihi* | *Tarehe* |
|---|---|---|---|
| T R BALAJI RAO | MKURUGENZI MKUU | (IMESAINIWA) | 18-03-2021 |
| FADHILI PETRO SANGA | MKUU WA FEDHA | (IMESAINIWA) | 18-03-2021 |
| FREDRICK HIPPOLITE | MKAGUZI MKUU WA NDANI | (IMESAINIWA) | 18-03-2021 |

**Sisi tuliotajwa hapo chini wajumbe wa bodi ya wakurugenzi tunathibitisha usahihi wa taarifa za hapo juu,tunatamka kwamba tumezitathmini taarifa hizi na kwa uelewa na imani yetu kubwa zimeandaliwa kulingana na Viwango vya Kimataifa vya Uwasilishaji wa Taarifa za Fedha na matakwa ya Sheria ya Benki na Taasisi za Fedha ya mwaka 2006 na zinaonesha hali halisi.**

| *Jina* | *Cheo* | *Sahihi* | *Tarehe* |
|---|---|---|---|
| 1. RAJAB S KAKUSA | MKURUGENZI | (IMESAINIWA) | 18-03-2021 |
| 2. INDIAEL DANIEL KAAYA | MKURUGENZI | (IMESAINIWA) | 18-03-2021 |
| 3. MWANAIDI A MTANDA | MKURUGENZI | (IMESAINIWA) | 18-03-2021 |

Canara Bank (T) Ltd
Head Office Dar Es Salaam Branch
Elia Complex P.O. Box 491, Dar Es Salaam, Tanzania
E:mail ctbl@canarabank.co.tz, T +255 222112530 (D) +255 222112532
www.canarabank.co.tz

## MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Uteuzi wa Mpango unatia matumaini

**RAIS** Samia Suluhu Hassan, jana alitegua kitendawili, alipomteua Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mpango kuwa Makamu wa Rais, hivyo kumaliza mjadala uliokuwa umeshika kasi kuhusu mtu atakayeshika nafasi hiyo.

Uteuzi huo umefanywa kujaza nafasi hiyo ambayo ilikuwa ikishikiliwa na Rais Samia aliyeapishwa kuwa rais kufuatia kifo cha Hayati Dk. John Magufuli, Machi 17, mwaka huu.

Katika mitandao ya kijamii na kwenye baadhi ya magazeti majina kadhaa ya wanasiasa yalikuwa yakitajwa, huku ikielezwa kuwa mmoja wao angeteuliwa kushika wadhifa huo mkubwa katika taifa letu.

Baada ya uteuzi wa Dk. Mpango jana, jina hilo liliwasilishwa bungeni asubuhi na kupigiwa kura na wabunge, ambao walimthibitisha kwa kura 363, sawa na asilimia 100, hivyo kudhihirisha kwamba uteuzi wa Rais kwa kushauriana na chama chake (CCM) ulikuwa sahihi.

Baada ya uteuzi huo na baada ya kuthibitishwa na Bunge, wengi walimwelezea Dk. Mpango kwamba ni mtu sahihi, huku wakimwelezea kuwa ni mtu wa Mungu, mwadilifu, mchapa kazi na sifa nyingine nyingi ndani na n je ya Bunge.

Hata yeye alipozungumza bungeni kabla ya kuthibitishwa, alidhihirisha jinsi gani anaguswa sana na matatizo yanayoikabili nchi yetu hususan umaskini na utayari wake wa kumsaidia Rais Samia kuyatafutia ufumbuzi kwa maslahi ya Watanzania wote.

Kikubwa aliahidi kumsaidia Rais Samia kuhakikisha miradi iliyoanzishwa na Dk. Magufuli utekelezaji wake utaendelea, huku pia akijinadi kwamba ni mchukia rushwa na udokoaji wa fedha za umma. Kadhalika aliahidi usimamizi wa rasilimali za umma na kwamba kwa hilo hana upole.

Tunampongeza sana Rais Samia kwa kumteua Dk. Mpango, ambaye ni mtumishi wa umma anayekidhi sifa karibu zote ambazo tuliziainisha kwenye safu hii Machi 25, mwaka huu za mtu anayefaa kuwa makamu wa rais.

Sifa tulizozieleza ni uadilifu, utiifu, kuchukia rushwa, kushehimu haki za binadamu, demokrasia, na utawala bora, mchapa kazi, mzalendo wa kweli, mbunifu, mwenye rekodi nzuri katika utendaji, mkomavu, mtulivu, anayeheshimika sana katika jamii, asiye na ubaguzi wa dini, rangi na itikadi za kisiasa.

Pia ambaye atamsaidia Rais Samia kutatua kero za wanyonge, kusimamia ukuaji wa uchumi, nidhamu ya utendaji na uwajibikaji serikalini, anayeweza kumsaidia kurejesha uhusiano mzuri na jumuiya ya kimataifa na asiye na matamanio ya kuunda mitandao kwa ajili ya kusaka uongozi wa juu wa nchi.

Tunathubutu kusema kwamba Samia ameonyesha kwamba kweli ni rais kama alivyosema wakati wa mazishi ya kitaifa ya Hayati Dk. Magufuli jijini Dodoma Machi 21.

Huu tunaona ni mwanzo mzuri katika uongozi wa Rais Samia, baada ya kumteua mtu ambaye ametoa utumishi wa kutukuka kwenye taifa letu na ambaye hajawahi kupata doa lolote. Tunampongeza sana Dk. Mpango kwa kuaminiwa na Rais Samia, hivyo amemteua kuwa msaidizi wake, ambaye pia atakuwa mshauri wake mkuu.

Tuna matumaini kwamba serikali itaendelea kutekeleza miradi yote ikiwamo ya kimkakati pamoja na kutoa huduma zingine muhimu za elimu, afya pamoja na kuwajali na kuwatatulia kero wanyonge.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Hongera Rais wetu, timu yako inazidi kuiva mtuonyeshe njia

Na Christina Mwakangale

**NCHI** ikiwa katika wiki ya pili ya maombolezo, shughuli zinaendelea kutekelezwa ikiwamo za kiserikali.

Serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan, baada ya utekelezaji kwa majukumu ya umma, imeanza mwishoni mwa wiki hii, baada ya kupokea ripoti ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

Kadhalika, Rais Samia, alipokea ripoti kutoka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU).

Kuanzia hatua alizozichukua baada ya ripoti za TAKUKURU na CAG, kumkabidhi ripoti, hatua hata maagizo aliyoyatoa, unatajwa na wachambuzi wa mbalimbali kwamba mwelekeo mzuri.

Jana, bungeni jijini Dodoma, bunge lilipokea jina la Makamu wa Rais, ambaye amependekezwa na Rais Samia, muda mfupi Spika wa Bunge, Job Ndugai, alimtangaza Dk. Philip Mpango kushika nafasi hiyo.

Ukizingatia hata aliyeteuliwa kuwa Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, anakiri yupo tayari kuhakikisha anasimamia maslahi ya taifa ili kulifikisha taarifa kwenye maendeleo.

Kwenye hotuba yake, Dk. Mpango anasema atamsaidia Rais Samia, katika majukumu yake ikiwamo kutoa ushauri pamoja na kudhibiti rushwa, kuhakikisha fedha za umma zinakuwa na matumizi sahihi.

Rais Samia, ambaye ni rais mwanamama wa kwanza kushika nafasi hiyo tangu uhuru wa nchi, macho yanaelekezwa kwake, ikiwamo matarajio.

Kwenye hotuba zake kadhaa kwa taifa, ikiwamo aliyoitoa baada ya kuapa na siku ya mazishi ya kitaifa, anauhakikishia umma kuwa atasimamia kiti hicho, ipasavyo bila ya kujali jinsia.

Anasema pamoja na nchi kupitia katika kipindi kigumu cha kuondokewa na Hayati Dk. John Magufuli, imani yake ushirikiano utadumu na amani kuwapo katika kuliendesha gurudumu la maendeleo la taifa.

Rais Samia, inawezekana ikawa ni mwanzo wa utekelezaji majukumu yake ikizingatiwa yaliyopo mbele pamoja na matatizo kwa wananchi kuwa mengi, atayafikia maeneo kadhaa.

Kuna maeneo ambayo yanatarajiwa kuimarishwa au kuboreshwa, hususan ajira kwa vijana, kundi ambalo ni kubwa nchini.

Kuwakumbuka vijana katika hilo, inaweza kuwa kwa kuwawezesha kwa kupata mtaji, kuboreshewa mazingira ya kujiajiri kwenye kilimo na ufugaji pia.

Walio wengi wana elimu ya kuwaongoza namna ya kufanya kazi zao baada ya kuhitimu masomo ya ngazi tofauti kuanzia ngazi za astashahada, stashahada na shahada, ingawa namna ya kujikwamua.

Kundi hili likijiajiri itakuwa ongezeko la pato kwa taifa ikizingatiwa wao ni nguvu kazi kubwa.

Pia kujikwamua kwao kutapunguza utegemezi, kwa kuwa hivi sasa vijana matarajio ni kinyume, wao ndio huwategemea zaidi wazazi au walezi wao.

Kuimarika kwa sekta binafsi ni fursa ya ajira kwa makundi yote, hasa yaliyo maalum ikiwamo wanawake, ambao hivi sasa kwenye kaya nyingi ndio vichwa vya familia.

Wajasiriamali wa shughuli tofauti za upishi, ushonaji usindikaji bidhaa na ubunifu tofauti unafanywa na makundi hayo ili kujiingizia kipato.

Wakati ikiwa ni mwanzo wa majukumu ya Rais Samia madarakani, yapo mengi yanayotarajiwa ambayo yatatoa mwanga kiuchumi, kisiasa, kielimu na sekta nyingine za kijamii, kwa taifa ambalo limeanza kukua baada ya misingi kuanzishwa na watangulizi wake walioliongoza taifa.

# TANGAZO

tigo pesa

ISSUED PURSUANT TO SECTION 34(3) (E) OF THE NATIONAL PAYMENT SYSTEMS ACT, NO 4 OF 2015 AND REGULATION 33 (B) OF THE ELECTRONIC MONEY REGULATIONS, 2015,

# THE REGISTERED TRUSTEES OF MILLICOM TANZANIA MOBILE SOLUTIONS

**Extracts from the Audited Financial Statements for the year ended 31 December 2020**

## STATEMENT OF PROFIT OR LOSS AND OTHER COMPREHENSIVE INCOMEFOR THE YEAR ENDED 31 DECEMBER 2020

| | Dec 2020 TShs' 000 | Dec 2019 TShs' 000 |
|---|---|---|
| Other income | 48,338 | 51,936 |
| Administrative expenses | (48,338) | (51,936) |
| **Profit before income tax** | - | - |
| Income tax | - | - |
| **Profit for the year** | - | - |
| Other comprehensive income | - | - |
| **Total comprehensive income for the year** | - | - |

## STATEMENT OF CASH FLOWS FOR THE YEAR ENDED 31 DECEMBER 2020

| | Dec 2020 TSh' 000 | Dec 2019 TSh' 000 |
|---|---|---|
| **Cash flows from operating activities** | | |
| Profit before tax | - | - |
| Changes in working capital: | | |
| Increase in deposits due to customers | 56,191,435 | 261,299,119 |
| Increase in abandoned deposits | 183,510 | 181,417 |
| **Cash inflows generated from operating activities** | **56,374,945** | **261,480,536** |
| **Net increase in cash and cash equivalents** | **56,374,945** | **261,480,536** |
| Cash and cash equivalents at 1 January | 261,480,536 | - |
| **Cash and cash equivalents at 31 December** | **317,855,481** | **261,480,536** |

## STATEMENT OF FINANCIAL POSITION AS AT 31 DECEMBER 2020

| | Dec 2020 TSh' 000 | Dec 2019 TSh' 000 |
|---|---|---|
| **ASSETS** | | |
| **Current assets** | | |
| Restricted cash | 317,855,481 | 261,480,536 |
| **TOTAL ASSETS** | **317,855,481** | **261,480,536** |
| **EQUITY AND LIABILITIES** | | |
| **Current liabilities** | | |
| Deposits due to customers | 317,490,554 | 261,299,119 |
| Abandoned deposits | 364,927 | 181,417 |
| **Total liabilities** | **317,855,481** | **261,480,536** |
| **TOTAL EQUITY AND LIABILITIES** | **317,855,481** | **261,480,536** |

The above extracts are from the Financial Statements of the Trust for the year ended December 31, 2020 which have been prepared in accordance with International Financial Reporting Standards. The Financial Statements were audited by Ernst & Young Certified Public Accountants (T) and received unqualified audit report.

These financial statements were approved by the Trustees on 30th March 2021 and signed by:

David T. Tarimo
**Trustee/Chairman**

Nelson E. Msuya
**Trustee/Vice Chairman**

Joseph C. Lyimo
**Trustee/Secretary**

**Head office**
Derm Complex, Kijitonyama
P. O. Box 2929
Dar es Salaam, Tanzania

# Awaua mke na mtoto kisha kujinyonga

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

JESHI la Polisi mkoani Kagera linafanya uchunguzi wa mtu aliyetajwa kwa jina la Sudi Muhamad kumuua mke na mtoto wake kisha naye kujinyonga.

Mtu huyo anadaiwa kujinyonga kwa kutumia shuka baada ya kufanya mauaji hayo.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Kagera, Revocatus Malimi, alisema tukio la mauaji hayo lilitokea Machi 25, mwaka huu, majira ya 3:00 usiku wilayani Muleba.

Alisema Muhamadi (49) mkazi wa Kijiji cha Mmayondwe, kabla ya kujinyonga, anadaiwa kuwa alikuwa na ugomvi wa kifamilia na mke wake, Editha Martine (48) baada ya mke wake kubadili dini.

Malimu alisema uchunguzi wa Polisi ulibaini kuwa chanzo ilikuwa ni mke na mtoto wake ambao wote ni marehemu walibadili dini kutoka uislamu kwenda ukristo na kuhama familia na kwenda kuishi sehemu nyingine.

"Mke alipobadili dini kulikuwa na ugomvi wa mara kwa mara. Mke huyo na binti yake ambaye naye ni marehemu, walihama nyumbani kwenda kuishi sehemu nyingine na ilipofika saa 3:00 usiku, mume alimshambulia mke wake kwa kumkata kwa panga sehemu mbalimbali za mwili," alisema Malimi.

Alisema wakati mtuhumiwa akikimbia sehemu ya tukio, alikutana na binti yake njiani na akaanza kumshambulia sehemu mbalimbali za mwili na kupoteza maisha.

Wakati huo huo, Malimi amesema jeshi hilo linamshikilia Msekwa Madaha (27) mkazi wa Kijiji cha Murongo wilaya ya Kyerwa, kwa tuhuma za kumpa ujauzito mwanafunzi wa darasa la nne mwenye umri wa miaka 15 (jina na shule vimehifadhiwa).

Kamanda Malimi alisema Machi 29, mwaka huu, majira ya 4:30 asubuhi, mwanafunzi huyo aligunduliwa na mwalimu mkuu wa shule aliyokuwa anasomea baada ya kufanya ukaguzi.

Alisema mwanafunzi huyo aligunduliwa kuwa na ujauzito wa miezi minne na alimtaja mhusika ambaye ni mtuhumiwa.



Wafanyabiashara wa kabichi, wakizishusha kutoka kwenye lori katika soko la Mburahati Madoto, jijini Dar es Salaam jana. Kiroba kimoja chenye kabichi 140 kinauzwa kwa 150,000/. **PICHA: MIRAJI MSALA**


## NOTISI / TANGAZO

**AUCTIONEERS AND PROPERTY MANAGERS CO.LTD, CHAMPION AUCTION MART LTD, SUNDI AUCTION MART LTD, SMARKCORE GROUP LTD, WAUNGWANA AUCTION MART LTD, MASETO AUCTIONEER AND DEBT COLLECTOR LTD, BEST GROUP LTD SALEI AUCTION MART LTD** kwa mamlaka tuliyopewa na Jamhuriya Muungano wa Tanzania, chini ya benki ya AKIBA COMMERCIAL BANK PLC, tunatoa notisi ya kulipa madeni kwa wadaiwa wafuatao ndani ya siku 14 kuanzia tangazo hili, Vinginevyo, tutafanya minada ya hadhara kama ratiba inavyoonyesha.

| TAWI HUSIKA | JINA LA MTEJA | JINA LA MDHAMINI | AINA YA DHAMANA | DHAMANA ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| MBEYA | MKINDO TRADERS LIMITED | AMOS GEORGE MAKALLA | GARI TOYOTA VX,T149 BDD | TABATA,DAR ES SALAAM | 20/4/2021 |
| MBEYA | KAJIGILI INVESTMENT COMPANY LIMITED | JOSEPH KAJIGILI MWANDOBOKA | GARI TOYOTA CANTER,T 178 DGQ | TABATA ,DAR ES SALAAM | 23/04/2021 |
| MBEYA | VENANCE JISKAKA MWAKYABALA | VENANCE JISKAKA MWAKYABALA | STORE NA FREMU ZA MADUKA ZENYE HATI MILIKI | MWANJELWA , MBEYA MJINI | 16/4/2021 |
| KARIAKOO | ABOUKBAKAR OMAR HASSAN | ABOUBAKAR OMAR HASSAN NA SAINECHA ABOUBAKAR OMAR | NYUMBA HATI NO. 113599/KIWANJA HATI NO. 105871/ | TEGETA NA KIBADA | 6/4/2021SAA 4:00 ASUBUHI NAKUENDELEA |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Mnunuzi atalazimika kulipa 25% ya bei ya nyumba au kiwanja papo hapo baada ya mnada kumalizika. Na 75% itakayo baki italazimika kulipwa ndani ya siku 14.
2. Ikiwa mnunuzi atashindwa kutimiza sharti lolote la mnada kuhusiana na malipo ya awali, hatarudishiwa pesa yoyote aliyokwisha ilipa.
3. Kwa mawasiliano zaidi; tupigie simu no. 0754497396 /0719922700
4. Iwapo ndani ya siku 60 mnunuzihajakabidhiwanyumba benki itarudisha kiasi cha fedha kilicho wekwa na mnunuzi benki bila gharama yeyote.


# Waziri aonya maofisa lugha za vitisho

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais Uwekezaji, Prof. Kitila Mkumbo, amewaonya baadhi ya watumishi wa serikali wenye tabia za kutoa kauli za vitisho kwa wawekezaji na wafanyabiashara ambao wanafika maeneo yao ya kazi kutaka kufanya uwekezaji.

Prof. Mkumbo, alisema hayo juzi mjini hapa wakati akifungua kikao kazi cha maofisa wa dawati wa utekelezaji wa programu ya kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji.

Alisema viongozi wa ngazi za juu wamebadilika na kukaa mkao wa kuwataka wawekezaji kwa wingi, hivyo lazima sasa maofisa wa ngazi za chini kubadili mtazamo katika suala la uwekezaji.

Alisema nchi lazima ijiweka kwenye ushindani kupitia msingi ya uwekezaji kwa kuwa ndiyo njia ya kukuza uchumi na haiwezekani kutoa huduma kama hakuna uchumi na Tanzania inatoa huduma kwa sababu kuna uwezekano wa uchumi kukua zaidi kupitia uwekezaji.

Kwa mujibu wa Sheria ya Uwekezaji ya mwaka 1997 ambayo itafanyiwa marekebisho, pamoja na mengine, alisema itaweka mazingira ya muundo juu ya ajira kwa Watanzania na wale wanaotoka nje.

Waziri Mkumbo alisema serikali imejikita katika kuwawekea mazingira mazuri ya kibiashara wawekezaji wa ndani na nje, hivyo mamlaka zilizopewa dhamana na serikali zinapaswa kuhakikisha katika utekelezaji wa majukumu yao, wanasaidia kuvutia zaidi wawekezaji.

# Upimaji ardhi kufanywa kumaliza migogoro ardhi

**Na Julieth Mkireri,** CHALINZE

KIJIJI cha Chamakweza kilichoko Kata ya Vigwaza, Halmashauri ya Chalinze, kitapewa kipaumbele kwenye upimaji wa ardhi.

Hatua hiyo inatokana na mikakati ya halmashauri, ambayo hivi karibuni imepatiwa vifaa vya kisasa vya upimaji wa ardhi kwa lengo la kupima ardhi ili kuondoa migogoro katika vijiji na vitongoji vilivyopo.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Kata ya Vigwaza, Shedeli Mikole, aliyasema hayo jana huku akimtaka Diwani wa Kata hiyo, Mussa Gama, kuhakikisha kijiji hicho kinakuwa cha kwanza katika upimaji huo.

Mikole alisema Chamakweza ni moja ya maeneo yenye mivutano ya ndani na mgogoro wa mpaka kati yake na Kitongoji cha Pingo, ambao nao unaelezwa kuwa ufumbuzi wake uko mbioni kupatikana.

Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Bagamoyo, Abdul Sharifu, alisisitiza Diwani wa kata hiyo kukutana na viongozi wengine wanaohusika kwa lengo la kufanikisha upimaji kwa haraka.

Gama aliwaeleza viongozi na wananchi walioshiriki katika kikao hicho kuwa Halmashauri ya Chalinze imepatiwa vifaa vya kisasa kwa ajili ya upimaji wa ardhi kwenye vijiji na vitongoji vyote ikiwa ni mpango wa matumizi bora ya ardhi.

Ester Moreto, mmoja wa wakazi wa Chamakweza, alisema kijiji hicho wanachoishi jamii ya wafugaji, kimekuwa katika migogoro ya ardhi kwa muda mrefu na Kijiji cha Pingo ambacho asilimia kubwa ya wakazi ni wakulima, hivyo endapo upimaji utafanyika utawasaidia kila mmoja kujua mipaka yake.

## TANGAZO

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
# WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI
## WAKALA YA BARABARA TANZANIA

Good roads for national development

# *SALAMU ZA PONGEZI*



**MHE. SAMIA SULUHU HASSAN**
**RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**



Mwenyekiti na Wajumbe wa Bodi, Mtendaji Mkuu, Menejimenti na Wafanyakazi wa **TANROADS,** tunakupongeza Mhe. Samia Suluhu Hassan kwa kuapishwa kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

**TANROADS** tunaungana na wapenda maendeleo wote kukutakia afya njema na mafanikio katika kuwatumikia Watanzania.

**TANROADS Makao Makuu:** **Ghorofa ya1-3, 10 Barabara ya Shaaban Robert / Garden Avenue S.L.P 11364 Dar es Salaam**
**BaruaPepe: Tanroadshq@tanrods.go.tz. www.tanroads.go.tz**

***MIUNDOMBINU BORA YA BARABARA NA VIWANJA VYA NDEGE KWA MAENDELEO YA TAIFA***

# Sababu kesi za ubakaji kukwama

BUNGE limeelezwa kuwa utafiti mbalimabli umefanywa na asasi mbalimbali za serikali na zisizo za kiserikali umebaini sababu mbalimbali za kutofanikiwa kwa baadhi ya kesi za ubakaji.

Miongoni mwa sababu hizo ni muhali, kumalizana nje ya mahakama, waathirika kuchelewa kuripoti vituo vya polisi.

Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Khamis Hamza Chilo, aliyasema hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la msingi la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Najma Murtaza Giga.

Mbunge huyo alihoji serikali inasemaje kuhusiana na ongezeko la vitendo vya ubakaji na udhalilishaji wa watoto nchini.

"Je, kwa nini serikali haifanyi utafiti kujua sababu za kesi nyingi kushindwa kuwatia hatiani wabakaji na kuja na mpango mpya wa kudhibiti vitendo hivyo," alihoji.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri huyo alisema kwa kipindi cha mwaka 2020 jumla ya washtakiwa 1,183

walihukumiwa vifungo jela.

"Ni wajibu wa serikali kuwalinda wananchi wakiwamo watoto dhidi ya makosa ya ubakaji na udhalilishaji. Ili kupambana na vitendo hivi serikali imekuwa ikichukua hatua kali ikiwamo kifungo cha miaka 30 jela kwa wanaojihusisha au kusaidia kufanyika kwa vitendo hivi," alisema.

Alitoa wito kwa wabunge na wananchi kwa ujumla kutoyafumbia macho matukio ya udhalilishaji na ubakaji ikiwamo kutoa taarifa kwa vyombo vya dola kwa wakati.

Katika swali la nyongeza, mbunge huyo alihoji serikali imejipangaje kuhakikisha vitengo vyote vinavyoshughulikia masuala ya sheria vinashirikiana kikamilifu ili kutokomeza masuala yaliyobainika kwenye utafiti.

"Je, mmekwama wapi katika kutekeleza sheria ya mtoto ambayo imeweka wajibu wa wazazi kuwalinda watoto juu ya ukatili?" Alihoji.Akijibu maswali hayo, Naibu Waziri huyo alisema serikali imekuwa ikitoa elimu kwa jamii kupitia vyombo mbalimbali ikiwamo madawati ya jinsia.

"Tumegundua sheria hii ipo kimadai zaidi kuliko kijinai na ndio maana inafika wakati utendaji kazi wa sheria hii ni mgumu sana, pia kuna ugumu wa utoaji wa ushahidi, mwisho wa siku sheria inakosa nguvu," alisema.

Katika swali jingine la nyongeza la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Ritta Kabati, alisema vitendo vya ubakaji katika Mkoa wa Iringa vimekithiri na wanaofanya vitendo hivyo wanaweka mawakili wasomi na wanashinda huku wasio na uwezo wakishindwa kuweka mawakili.

Akijibu swali hilo, Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Mwigulu Nchemba, alisema serikali imeweka utaratibu wa kuwapatia msaada wa kisheria wasio na uwezo wa kuweka mawakili kwenye kesi hizo.

Alisema wapo kwenye hatua za mwisho za mazungumzo katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Ofisi ya Rais-TAMISEMI, ili kuwatumia wanasheria waliopo chini ya halmashauri kuwasaidia wananchi kupata msaada wa kisheria.



Baadhi ya wabunge wakiingia bungeni kwa ajili ya kuanza kikao cha kwanza cha Bunge la 12, mkutano wa tatu, jijini Dodoma jana. PICHA: IBRAHIM JOSEPH

# Bil. 3/- kusambaza mbegu za michikichi

SERIKALI imesema katika mwaka 2021/22, imetenga Sh. bilioni 3.15, kwa ajili ya kuzalisha na kusambaza mbegu na miche ya zao la michikichi ili kukabiliana na mahitaji ya mafuta ya kula nchini.

Naibu Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, alitoa kauli hiyo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Kigoma Kaskazini (CCM), Assa Makanika.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji serikali haioni umuhimu wa kuwekeza yenyewe katika zao la michikichi badala ya kuziachia halmashauri ili kukabiliana na upungufu wa mafuta nchini.

Bashe akijibu swali hilo, alisema katika kipindi cha mwaka 2019/20 hadi mwaka 2020/21, imewekeza Sh. bilioni 5.8 kwa ajili ya kuendeleza zao la michikichi.

Aidha, alisema hadi kufikia Januari 31, mwaka huu, jumla ya miche bora ya michikichi 2,244,935 imezalishwa na jumla ya miche 1,456,111 imesambazwa kwa wakulima katika Halmashauri za Wilaya za Mkoa wa Kigoma.

"Miche 788,824 inatarajiwa kusambazwa kwa wakulima katika msimu wa 2020/2021," alisema.

Naibu Waziri huyo alisema mahitaji ya mafuta ya kula nchini yanakadiriwa kuwa tani 570,000 kwa mwaka.

Hata hivyo, alisema uzalishaji wa mafuta ya kula nchini unakadiriwa kufikiwa wastani wa tani 205,000 na kufanya upungufu wa wastani wa tani 365,000 kwa mwaka, ambapo hupelekea nchi kutumia wastani wa kiasi cha Sh. bilioni 474 kuagiza mafuta ya kula kutoka nje kwa mwaka.

"Kama ilivyo kwa mazao mengine, serikali huwekeza katika utafiti, uzalishaji na upatikanaji wa pembejeo za kilimo, huduma za ugani, udhibiti wa visumbufu vya mazao na utafutaji wa masoko," alisema.

Aidha, alisema katika utekelezaji mikakati hiyo, serikali imekuwa ikishirikiana na wadau mbalimbali zikiwamo Mamlaka za Serikali za Mitaa na sekta binafsi.

"Kama sehemu ya mkakati wa kujitosheleza kwa mafuta ya kula, mwaka 2018 serikali iliamua kuanzisha kituo maalum cha utafiti wa zao la michikichi cha TARI Kihinga mkoani Kigoma ili kuendeleza zao hili kwa ufanisi zaidi," alisema.

Alisema TARI Kihinga inashirikiana na Wakala wa Mbegu za Kilimo (ASA), halmashauri na sekta binafsi katika utafiti, uzalishaji wa miche bora ya michikichi na kuisambaza kwa wakulima.

"Serikali itaendelea kushirikisha wadau wa sekta ya umma na binafsi kuendeleza zao la mchikichi na mazao mengine ya mbegu za ili kuwezesha nchi kujitosheleza kwa mafuta ya kula," alisema.

# TANESCO kuwezeshwa kuboresha miundombinu

WIZARA ya Nishati imesema itaendelea kuliwezesha fedha Shirika la Umeme nchini (TANESCO), ili kuboresha miundombinu ili kuwa na umeme wa uhakika.

Naibu Waziri, Stephen Byabato, alibainisha hilo bungeni jana alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Viti Maalum, Esther Matiko, aliyetaka kujua ni lini serikali itahakikisha kunakuwapo na umeme wa uhakika.

Byabato alisema umeme upo na unaendelea kuongezwa kupitia utekelezaji wa miradi mbalimbali ili kufikia kila mwananchi.

Katika swali la msingi, Mbunge wa Handeni (CCM), Reuben Kwagilwa, alihoji ni lini wananchi katika mitaa 30 isiyo na umeme wilayani Handeni watapatiwa umeme kupitia mradi wa umeme vijijini (REA).


Akijibu swali hilo, Naibu Waziri huyo alisema serikali kupitia TANESCO na REA inaendelea kutekeleza mradi wa kusambaza umeme katika vijiji, mitaa na vitongoji visivyo kuwa na umeme kupitia miradi mbalimbali.

"Kwa sasa Mkandarasi Kampuni ya M/S Sengerema Engneering Ltd amepewa kazi ya kupeleka umeme katika vijiji 15 na mitaa na vitongoji zaidi ya 30 katika Wilaya ya Handeni," alisema.

Aidha, alisema kazi hizo zinajumuisha ujenzi wa njia ya umeme ya msongo wa kilovoti 0.4 umbali wa kilomita 27.5, ufungaji wa transfoma 11 za 50kVA na 100kVA, pamoja na kuwaunganishia umeme wateja wa awali 669.

"Mradi unakadiriwa kugharimu Sh. bilioni 3.36, utekelezaji wa mradi umeanza Februari, 2020 na utakamilika ifikapo Desemba, 2022,"alisema.

Aidha, alisema TANESCO inaendelea kuunganisha umeme wateja ambao hawajaunganishwa umeme katika mitaa na vitongoji vya Tanzania Bara ikiwamo Wilaya ya Handeni kupitia majukumu yake ya kila siku.




Habari na Augusta Njoji






Ukurasa 14

DENIS SASSOU-NGUESSO

## Kashinda tena akianza safari ya miaka 41 urais, umri miaka 77



Ukurasa 13

## JPM alivyopanua wigo wa uelewa katika namna ya kuongoza Afrika

siasa

JUMATANO MACHI 31, 2021

HABARI BORA NA KAMILIFU

Nipashe

# Jicho linavyoangazia 'hapa kazi' ya Rais mpya na ugeni Makamu wake

• Dk. Slaa: Niliwafahamu hivi miaka 25 na JPM

**Sabato Kasika na Anthony Gervas,** MWANZA

HUYO ndiye Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, aliyeanza kuonyesha uhalisia wa umahiri, stadi na jinsi anavyotaka kazi ifanyike kwa ajili ya maendeleo ya nchi hii.

Ni jambo linaloonekana mara tu baada ya kupokea Ripoti ya Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali na kuisoma, siku inayofuata alipopokea rasmi, kisha alijijibu kwa kukunjua makucha, akihoji uhalali wa baadhi ya matumizi katika ofisi za serikali.

Ushuhuda tayari upo, wapo waliosimamishwa kazi kuwajibikia hoja za kisheria kuhusu matumizi ngazi ya mabilioni ya fedha za umma, pale alipopokea ripoti za taasisi za umma kutoka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Umma (CAG) na Taasisi ya Kuzuia na Kupamabana na Rushwa (TAKUKURU).

Ni hatua inayomuakisi Rais Samia ni kiongozi wa aina gani, katika aina ya 'salamu' hataki ubabaishaji kazini, wanaokwamisha maendeleo ya Tanzania.

Katika kupokea ripoti hizo, mbali na kuongeza dai la ufanisi kiutendaji, pia akamnyooshea kidole waziri mwingine kutokubaliana na 'madudu' katika maeneo yake ya kazi, akitaka kuwapo usahihi. Ni ishara kwamba hana mzaha bali kuchapa kazi kwa ajili ya maendeleo ya Tanzania na watu wake.

Saa chache, waziri naye akachukua hatua kadhaa, kule alikonyooshewa kidole. Ahadi ya 'hapa kazi tu' inaendelea kwa vitendo.



Hayati Dk. John Magufuli, alipokuwa na Balozi Dk.Willibrod Slaa. **PICHA: MTANDAO**

**UTEUZI MAKAMU RAIS**

Vilevile, ni jana tu Rais Samia aliendelea kuonyesha kuwa anataka kufanya kazi na watu wa aina gani, baada ya kumpendekeza Dk. Philip Mpango kuwa Makamu wa Rais, akiamini ndiye anayeweza kumsaidia katika nafasi hiyo.

Dk. Mpango amekuwa Waziri wa Fedha kwa kipindi cha miaka mitano mfululizo tangu alipoteuliwa na Rais Hayati akiwa mbunge asiye na jimbo, Dk. John Magufuli na akamteua tena, baada ya uchaguzi mkuu wa mwaka jana.

Jana saa 6.32, Spika wa Bunge Job Ndugai, alitangaza kupitishwa kwa asilimia 100, jambo ambalo mbali na kumtakatisha Dk. Mpango aliyeaga rasmi kwa kutoka bungeni jana saa 6.35 akiwa amevua ubunge wa Buhigwe kikatiba, vivyo hivyo kauvua uwaziri wa Fedha.

Samia Suluhu Hassan, aliyejionyesha rasmi kwa matendo kwamba yeye ni kiongozi wa aina gani, utendaji kazi wake na aina ya makundi watakaofanya kazi naye.

Hata pendekezo lake la uteule lina wasifu ambao Dk. Mpango aliwekeza, ikiwamo utiifu.

Binafsi anakiri wasifu aliyopewa bungeni wa 'upole' ila akataja sura yake ya pili iliyojificha ya ukali na huonekana pale anapokuwa katika jukumu la kumsaidia Rais Samia, anaona maslahi ya Tanzania yanachezewa.

Mhadhiri wa Chuo cha Diplomasia jijini Dar es Salaam, Abbas Mwalimu ni mchambuzi wa siasa, ana maoni yake kuwa:"Tayari mama Rais Samia Suluhu Hassan ameshatuma ujumbe wa kuwaondoa wasiwasi Watanzania kuwa Dk. Magufuli amemaliza kazi iliyomleta duniani ya kumwonyesha namna kazi zinavyofanywa."

Anafafanua, kwa sasa Rais huyo wa awamu ya sita, anajua namna ya kutekeleza na kuchukua uamuzi mgumu kwa maslahi ya taifa kwa kufuata njia hiyo ambayo Dk. Magufuli ameiacha.

INAENDELEA UK.12

# Jicho linavyoangazia 'hapa kazi' ya Rais mpya na ugeni Makamu wake

INATOKA UK.11

Anafafanua kuwa, serikali imekuwa katika mikakati ya kuboresha huduma za jamii, ujenzi wa miundombinu mbalimbali, miradi ya maendeleo na sera zake za kiuchumi, mambo ambayo rais mpya anasisitiza kufuata nyayo za mtangulizi wake kwa masilahi ya taifa hili.

**UMOJA & MSHIKAMANO**

Katibu Mkuu wa Chama cha ACT- Wazalendo, Ado Shaibu, anasema, rais ameshawahakikishia umma kuwa hakuna jambo litakaloharibika, kwa vile nchi iko katika mikono salama na kwamba yeye na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, wataendeleza alipoishia Dk. Magufuli, hata kufika walipopatamani.

"Kimsingi, katika hotuba yake kule Dodoma, Rais wa awamu ya sita, Samia Suluhu Hassan, alikuwa anawaondoa wasiwasi Watanzania kuwa yale mazuri yaliyofanyika enzi za Dk. Magufuli kwamba atayaendeleza," anasema Ado.

Anasema, Rais pia amedhihirisha hekima zake kwa kutambua umuhimu wa wazee kwa kuwaambia viongozi wastaafu kwamba anahitaji mchango wao katika uongozi wake.

"Hii inaonyesha ni jinsi gani anawasilisha ujumbe kuwa uongozi wake unahusisha busara za watangulizi wake, viongozi wastaafu wa chama na serikali kutoka pande zote za Tanzania," anasema.

Anasema, Rais ananyenyekea kwa kuwaomba wazee pande zote za Muungano na viongozi wastaafu kuwa yeye ni kijana wao kama alivyokuwa Dk. Magufuli na yupo tayari kushirikiana nao bega kwa bega katika kujenga Tanzania aliyotamani Hayati Magufuli na wanayoitamani Watanzania.

**JICHO LA DK. SLAA**

Balozi wa Tanzania nchini Sweden, Dk.Willibrod Slaa, aliyekwishawahi kuwa kigogo wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), anaeleza kumfahamu kwa mara ya kwanza Hayati Dk. John Magufuli, baada ya kukutana kwa mara ya kwanza bungeni jijini Dodoma.

"Nilimfahamu hayati Rais, tulipoingia wote bungeni kwa mara ya kwanza jijini Dodoma mwaka 1995, akitokea jimbo la Chato, wakati huo ilikuwa mkoa wa Mwanza na mimi nikitokea Jimbo la Karatu mkoani Arusha," anasema Dk.Slaa.

Anafafanua kuwa, walifanya kazi wote kwa ushirikiano bungeni, pia Dk. Magufuli alikuwa akimtembelea Dk. Slaa jimboni kwake Karatu na hakuwahi kuwabagua, kutokana na tofauti zozote walizokuwa nazo.

"Hayati Dk. Magufuli ni mtendaji kazi. Yeye kama mtu hana nidhamu, huwezi kufanya naye kazi. Vilevile ukiwa hauna kasi ya utendaji wala kujua malengo yake katika nafasi aliyokupangia, hutaendana naye," anasimulia.

Dk. Slaa anasema, alithibitisha hilo kwamba ni pale alipoteuliwa katika nafasi ya kuwa balozi nchini Sweden, alipewa kipimo cha kurejesha ripoti kwa maandishi.

Anasema aliteuliwa kwa nafasi hiyo akiwa hana chama chochote cha siasa, baada ya kujiuzulu katika nafasi yake ya Katibu Mkuu wa CHADEMA na hadi sasa si mwanachama.

Dk. Slaa anakiri kwa mifano kuwa hajaona ubaguzi wa aina yoyote kazini na nje ya nchi, iwe hata katika siasa, hali aliyodhihirisha hata kwa wateule wenzake kutoka kambi ya upinzani kama Dk. Anna Mghwira, Mkuu wa Mkoa na Profesa Kiyiola Mkumbo, nafasi ya uwaziri.

Anamsifu Hayati Dk. Magufuli alimsifu katika sura ya utu, urafiki na hakuwa kiongozi wa maneno, bali alimtaka mchapa kazi na adui kwa walioonekana wala rushwa na wazembe wa kazi.

Pia anasema amekuwa akiwafuatilia wabadhirifu wa fedha za serikali, alipowakemea bila kuogopa, ikiwamo 'kuwatumbua' pasipo kujali urafiki.

Balozi Dk. Slaa, anasimulia kuwa baada ya kuteuliwa kuwa Balozi nchini Sweden, akiwa na wenzake walipewa, vipengele vya kuwapima utendaji kazi wao, kuhakikisha wanatuma ripoti kwa maandishi ya utendaji kazi, kila baada ya miezi mitatu.

Anasema baada ya kutuma ripoti hiyo anayoitaja ya kurasa 30, Hayati Dk. Magufuli alikuwa akiisoma kila kurasa, kujiridhisha na kile alichotumwa kwenda kukifanya.

Dk. Slaa anamsifu kiongozi huyo aliyekuwa mkuu wa nchi, kwamba aliweka rekodi bora, kutokana na kuwasikiliza, hata barabarani alipokuwa ziarani na kutatua kero pale pale, katika staili ya kuchukua uamuzi mgumu, ikiwamo pale 'alipomtumbua' Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri mojawapo. Hapo anathibitisha kifo chake ni pigo kwa taifa.

**ALIVYOMFAHAMU SAMIA**

Dk. Slaa anafungua ukurasa wa pili, kuhusu namna alivyomfahamu Rais Samia Suluhu Hassan, pale mama huyo alipoteuliwa mwaka 1996 kuwa Balozi wa Kuhamasisha na Kutoa Elimu ya Ugonjwa wa Fistula, ambao unawatesa kinamama wengi.

Anasema, Rais Samia alikuwa akihamasisha uelewa kwamba ni ugonjwa unaotibika akipinga vikali dhana kwamba ni mkosi au uchawi.

Dk. Slaa anafafanua imani yake kwamba, Rais huyo ana nafasi bora ya kuiongoza Tanzania na kusimamia miradi ya wananchi kwa ufanisi, kwa sababu amefundishwa utendaji kazi bora na mtangulizi Dk. Magufuli, pale waliposhirikiana kuiongoza serikali.

Anawahakikishia Watanzania kuwa, Rais Samia ana uwezo wa kuchapa kazi na ndiyo maana aliteuliwa kuwa Makamu wa Rais aliyetangulia.

Dk. Slaa, anahitimisha kwa kumbebesha Rais Samia wasifu tatu za; mtu makini, mwenye moyo wa huruma na upendo kwa wananchi, hivyo wananchi wanatakiwa kumuunga mkono katika kulisukuma mbele gurudumu la maendeleo aliloachiwa.



Rais Samia Suluhu Hassan. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

> Hii inaonyesha ni jinsi gani anawasilisha ujumbe kuwa uongozi wake unahusisha busara za watangulizi wake, viongozi wastaafu wa chama na serikali kutoka pande zote za Tanzania.



Balozi Dk. Willibrod Slaa.

UCHAMBUZI

# JPM alivyopanua wigo wa uelewa katika namna ya kuongoza Afrika

Na Nimi Mweta

• Yasiyowezekana, amefanya yawezekane




Hayati Rais John Magufuli, akiwa kwenye kikao cha kimataifa enzi za uhai wake. **PICHA: MTANDAO**

IKO bayana kila kona, kifo cha Rais wa Tanzania, Dk. John Magufuli, kimeishtua Bara la Afrika. Sasa ni wiki mbili hatunaye katika wakati wa kutafakari mchango wake katika sura au aina ya Afrika inayostahili kwa undani zaidi, eneo hilo likiwa sura pana ya dunia kwa jumla.

Mwasisi wa Taifa Mwalimu Nyerere, awali alishaonyesha upana wa kile kinachowezekana, endapo kuna mwenye dhamira ya dhati na uelewa wa kina wa kile anachotaka kufanya.

Kuna wasomi Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, wanaeleza kuwa katika vyuo vikuu ng'ambo vyenye idara za utafiti kuhusu Afrika, maprofesa wao wamegawanyika katika makundi makuu mawili, wanaoumuunga mkono na wanaompinga Mwalimu Nyerere.

Hapo Dk. Magufuli amelinganishwa Edward Sokoine, aliyekuwa Waziri Mkuu katika zama za Mwalimu Nyerere kwa vipindi viwili vifupi, mwanzoni mwa miaka ya 1980, kabla ya kufariki dunia Aprili mwaka 1984.

Ila kuibadili sura ya nchi na kujenga miundombinu na hata misingi halisi ya maendeleo, ni kazi inayohitaji muda na hasa mwenye maono na taswira hiyo anapokuwa ndiye kiongozi mkuu wa nchi. Ndivyo alivyokuwa JPM.

Kwa maana hiyo, alikuwa na nafasi ya kipekee, bila ya kuwa na muda mrefu madarakani, miaka sita tu, kwa kifupi ni Rais aliyekaa kipindi kifupi zaidi madarakani, huku Mwalimu Nyerere, aliyekaa kwa muda mrefu zaidi wa miaka 24.

Hata hivyo, akiwa hayuko duniani kwa wastani wa wiki mbili sasa, anabaki na historia ya ufanisi wa hali ya juu, akiibadilisha haiba ya nchi kwa kiwango kikubwa na sura pana katika aliyotarajia na chama chake.

Moja ya maeneo yaliyowashangaza hata wale wanaodhani wanaifahamu vyema Tanzania na Afrika kwa jumla, ni suala la 'kutumbua majipu' katika hali kinyume kabisa na matazamo ya wenye madaraka katika maeneo takriban yote ya utawala.

Hapo kuna utumishi serikalini, mamlaka za kusimamia sekta tofauti za uchumi na mashirika ya kibiashara, ambako serikali ina hisa, maeneo yenye asili ya kujitegemea kwa kiwango fulani na kutazamia kuwa serikali itapokea maombi ya misaada kutoka hazina, pale wanapokuwa na upungufu kadhaa. Hapa kutazamiwa, kama serikali ingehoji sana 'kulikoni.'

Katika namna ya mwendelezo wa itikadi za Mwalimu Nyerere, hakuwa mpenda fedha na aliyechukia rushwa, Dk. Magufuli naye alishangaza watu alipowaonyesha uwezo kwamba 'rushwa siyo mfupa uliomshinda fisi.'

### BAADA YA MIAKA

Katika zama hizo za miongo zaidi ya minne iliyopita na hata kabla ya hapo, historia iko bayana kuna wasomi walikuwa wachache waliotokea vijijini moja kwa moja kuingia shuleni na waliobahatika kuendelea wanaohesabika.

Historia inasonga mbali, kwamba waliobahatika kuviona vyuo ambaye tena kwa kuvitaja Makerere na baadaye kuanzishwa cha Dar es Salaam, hawakuwa tu watumishi wa umma, ila ni nyota za maeneo wanakotoka. Mwalimu alielewa hali hiyo.

Ila hatua ya leo katika hesabu ya awamu ya kwanza ya uongozi wa nchi, hadi ya tano kuna kile Waingereza wana usemi 'maji mengi yamepita chini ya daraja.'

Ni aina ya mabadiliko yenye taswira yake. Wasomi wanaofanya kazi serikalini au mashirika ya umma, wanajiwakilisha na siyo tena makabila au jamii zao kama ilivyokuwa historia za huko nyuma.

Matokeo yake ni kwamba, dola inakua na uwezo wa kumwajibisha mtendaji kivyake, pale anaposema iwe kwa nidhamu, ubadhirifu au uzembe.

Mtu huyo hana uwezo wa kukimbilia kwao na kutoa malalamiko kwa wazee, waanze 'kuichunia' serikali, kutoshiriki uhamasishaji wa mambo yake, kama ilivyokuwa mwanzoni penye mzizi wa historia, msingi unaomwezesha kiongozi mwenye nia thabiti kusafisha ubadhirifu serikalini mwake.

Uthubutu wa kupambana na rushwa, umejenga taswira mpya kuhusu uwezo wa serikali katika bara Afrika, kwa kuzingatia demokrasia nayo inaota mizizi, huku pingamizi zake kama mifungamano ya kabila na dini katika jamii inapungua.

Suala la kudhibiti rushwa serikalini, inayojumuisha mustakabali wa mambo kama wizi, ubadhirifu, kuchota fedha wanazolipwa 'wafanyakazi hewa,' kuingiza jamaa za watendaji kwa kutumia vyeti feki, unatokana na utumiaji vyema rasilimali za serikali na kukidhi matazamio ya wapigakura.

Wanaokwama katika nafasi zao kutokana na kubanwa na kiongozi wa nchi, wanashindwa kuchochea mkondo tofauti wa hisia, kwani wananchi wanaridhika na utendaji serikalini, kiwango ambacho kwa jumla kilidhaniwa hakiwezekani, au hakikuwahi kufikiriwa.

Hapo ndio penye ada ya kuwa mwanamapinduzi, anaupelekea umma katika upeo mwingine na kufuatilia kudhihirisha kuwa 'inawezekana, ukifanya wajibu wako,' alivyosema Nyerere mwaka 1964.

Pia kuna sura za mikwamo mingi ya uendeshaji dola barani Afrika, mfano ni katika baadhi ya nchi kunakuwapo wanaoziongoza wakidumu zaidi ya miaka 30. Ni namna inayochangia kujengea Afrika taswira hasi mbele ya bara nyinginezo kama za Bara Ulaya na Marekani.

### WAUONAVYO UJAMAA

Kuna wakati, Rais aliyepita wa Marekani, Donald Trump, alishatamka alipoingia madarakani mwaka 2017, kuwa hataki wahamiaji wanaokimbia, akipatolea dhana yenye lugha ya kudhalilisha.

Mwalimu Nyerere akiondoka madarakani mwaka 1985, uchambuzi wa siasa nchini Marekani, mzaliwa wa Kenya na kasomea Uingereza, Profesa Ali Mazrui, alishasema katika miaka ya nyuma kuwa Ujamaa 'ilishindwa kishujaa.'

> Kuwapo vihunzi kama mafuta ghafi yalipanda bei mara kadhaa kati ya Oktoba 1973 na Oktoba 1974, bidhaa za matumizi zikaongezeka, hali iliyoumiza uchumi wa nchi.

Anasema, ilikuwa jitihada ya kuthubutu kubuni mpango wa kurekebisha maisha ya taifa na kuweka itikadi mpya iliyotazamiwa kuwa na tija na ufanisi, lakini nchi zilikuwa mtegoni.

Matazamio ya uchumi ya wakati ule, anasema yalilenga kuuza mazao nje kwa bei nzuri na viwango vya kubadilishana fedha, kuwa thabiti kuwezesha kununua vianzio vya kujenga viwanda.

Kuwapo vihunzi kama mafuta ghafi yalipanda bei mara kadhaa kati ya Oktoba 1973 na Oktoba 1974, bidhaa za matumizi zikaongezeka, hali iliyoumiza uchumi wa nchi.

Pia katika historia ya uchumi ni kati ya miaka ya 1997-2007, uchumi wa madini hasa dhahabu ulikuwa umepanda, uwekezaji katika utalii ukafikia kiwango cha juu na ugunduzi wa gesi asilia ukapunguza mzigo wa kununua mafuta kutoka nje, yakiwa tayari yamesafishwa.

Ni katika zama uwezo wa kiuchumi ulikuwa unakua kwa kasi, kwa mfano Bajeti ya Taifa Mwaka 1998 ilikuwa Sh. trilioni 1.1, fedha za nyumbani zikiwa Sh. bilioni 720, wakati miaka 20 baadaye (akiwa madarakani JPM) ujazo wa Bajeti ya Taifa ukawa tayari ni mara 30 kwa fedha za ndani.

Uwezo wa nchi za nje, wenyewe haukuwa unaongezeka kwa haraka kiasi hicho, na serikali ikawadhibiti katika eneo la madini, kwanza.

JUKWAA LA UONGOZI

DENIS SASSOU-NGUESSO

# Kashinda tena akianza safari ya miaka 41 urais, umri miaka 77

**Na Christina Mwakangale**

RAIS Sassou Nguesso (77) ni kati ya viongozi waliokaa madarakani kwa muda mrefu barani Afrika akiwa nchini Congo-Brazaville, taifa lenye utajiri mkubwa wa mafuta.

Hapo anafanana sana na Yoweri Museveni, nchini Uganda ambaye kamaliza miaka 34 ya uongozi na kashinda uchaguzi mwaka jana akisonga katika miaka 38 madarakani.

Sassou-Nguesso, hivi karibuni ameshinda tena katika uchaguzi nafasi ya urais, akiwa amekaa madarakani takribani 36, kwa vipindi tofauti, kwa kuwa kuna awamu alishindwa.

Tangu 1979 ameongoza nchi, isipokuwa aliposhindwa katika uchaguzi wa mwaka 1992. Katika uchaguzi uliofanyika mwezi huu, Sassou-Nguesso amepata ushindi kwa asilimia 88.57 ya kura kwa kipindi cha miaka mitano ijayo.

Alipambana na wagombea saba kutoka vyama vya upinzani. Sassou-Nguesso, mbali na kukaa muda mrefu madarakani kama rais wa nchi, alionyesha kushinda kila maeneo ya nchi.

**MATOKEO HAYO**

Tume ya Uchaguzi nchini humo ilimtangazia ushindi wa asilimia 88.57, huku mwaka 2016 walipata asilimia 60.19 ya kura.

Kuna wagombea wa upinzani sita walioshiriki mchakato huo wa urais katika kinyang'anyiro hicho, wakiongozwa na mpinzani mkuu, Guy-Brice Parfait Kolélas, ingawa kabla ya kutolewa matokeo rasmi, Kolélas. kilitangazwa kifo chake, akidaiwa kuugua Covid-19.

Matokeo ya Kolélas. Kwa mujibu wa tume, alipata kura nyingi, baada ya kupata asilimia 7.8. kwa upande wa upinzani.

Akifuatiwa na Waziri wa zamani wa Fedha, Mathias Dzon aliyepata asilimia 1.90 ya kura na wagombea wengine wako chini ya asilimia moja ya kura.


Wapinzani baada ya matokeo hayo walitangaza kuwasilisha malalamiko katika Mahakama ya Katiba. Washirika wa karibu wa Kolélas wamelaani wanachokiita udanganyifu mkubwa wa kura kwenye uchaguzi huo ambao umempa ushindi Sassou-Nguesso.

Mathias Dzon, kwa upande wake, alibaini kwamba uchaguzi huo ulikuwa haueleweki, huku wakiwa na siku tatu kuwasilisha malalamiko yao akiunga mkono kuwasilisha malalamiko mahakamani.

Hata hivyo, waangalizi wa Umoja wa Mataifa (UN) na Umoja wa Ulaya (EU) hawakualikwa kufuatilia uchaguzi.

**MAISHA KISIASA**

Kwa mara ya kwanza, Sassou-Nguesso alihudumu kama rais kati ya mwaka 1979 hadi 1992 alipomaliza utawala wake wa mihula mitatu chini ya mfumo wa vyama vingi.



Rais Denis Sassou Nguesso. **PICHA: MTANDAO**

> Sassou Nguesso alikuwa kiongozi wa upinzani kwa miaka mitano, kabla ya kurejea madarakani wakati wa vita vya pili vya wenyewe kwa wenyewe mwaka 1997 hadi 1999.

Nguesso alialichukua tena nchi mwaka 1997 baada ya vita ya muda mfupi vya wenyewe na waasi kumuondoa madarakani aliyekuwa rais Pascal Lissouba, akarejea madarakani.

Kipindi cha tatu katika uongozi wake alichaguliwa tena mwaka 2002 pia mwaka 2009, ikidhaniwa itakuwa muhula wake wa mwisho baada ya kukaa miaka saba madarakani.

Mwaka 2015 Sassou-Nguesso aliitisha marekebisho ya katiba yaliyoondoa ukomo wa umri wa miaka 70, kipengele, ambacho kingemzuia kuwania urais kwa mara nyingine, pia kufuta kipengele cha mihula miwili ya miaka saba madarakani na kuweka kipengele kipya cha mihula mitatu ya miaka mitano.

Uchaguzi wa mwaka 2016, baada ya kutokea vurugu ilikadiriwa watu zaidi ya 17 walipoteza maisha. Hapo ndipo wapinzani walimtuhumu Sassou-Nguesso, aliyepata ushindi wa asilimia 67 ya kura zote.

Kadhalika wapinzani wawili baada ya uchaguzi wa mwaka 2016, akiwamo Jean-Marie Michel Mokoko na Andre Okombi Salissa, walituhumiwa huku wakikutwa na hatia ya makosa ya kuhatarisha usalama.

**WAPINZANI WAKE**

Mapema, Januari mwaka huu, chama kikuu cha upinzani cha The Pan-African Union for Social Democracy (UPADS), kilitangaza kutoshiriki uchaguzi.

Chama hicho kilidai kwamba mazingira ya uchaguzi hayaridhishi na kupendekeza uchaguzi wa siku ya Jumapili, ufanyike mwaka 2023 na Rais Sassou Nguesso asiwe mgombea.

Kolelas aliyeteuliwa na Chama cha Union of Democratic Humanists (UDH-YUKI) kugombea kiti cha urais mwaka huu, alikuwa mpinzani mkuu wa Sassou-Nguesso.

Yumo pia, Mathias Dzoni, Waziri wa zamani wa Fedha chini ya utawala wa Nguesso, aliyegombea urais mwaka huu, ambaye uchaguzi wa mwaka 2016 alitangaza kutoshiriki akisema uchaguzi usingekuwa huru na haki.

Mwingine ni Albert Oniangue, ambaye ni mchungaji na aliwahi kutumikia jeshi la nchi hiyo kufikia ngazi ya cheo cha Kanali, amekuwa mgombea mpya katika siasa za nchi hiyo.

Wagombea wengine ni pamoja na Joseph Kignoumbi Kia Mbougou, Anguios Nganguia Engambe na Dave Mafoula mwenye umri wa miaka 38 na mgombea pekee kijana zaidi kwenye kinyang'anyiro cha urais, Congo, mwaka huu.

Pamoja na idadi hiyo wapinzani, wachambuzi wa mambo na viongozi wa mashirika ya kiraia nchini humo wanasema kati ya wagombea wote sita, hakuna ambaye ana uwezo wa kumwondoa madarakani Rais Sassou Nguesso.

**WASIFU WAKE**

Denis Sassou-Nguesso, alizaliwa mwaka 1943, mwanasiasa, kiongozi mstaafu wa jeshi aliyekitumika kiti cha urais mara mbili.

Sassou-Nguesso alijiunga na masomo ya sekondari ya Loubomo mwaka 1956 hadi 1961 na baada ya hapo, alijiunga na jeshi na kisha kwenda kwenye mafunzo ya kijeshi nchini Algeria na Ufaransa.

Mwaka 1963 Sassou-Nguesso alichaguliwa kuwa kamanda wa majeshi, miaka ya 1970, na kufikia kiwango cha kuwa Kanali na baada ya hapo, aliamua kujiunga na siasa.

Kadhalika, Sassou-Nguesso katika nafasi za uongozi kikanda, aliwahi kuchaguliwa kuwa mwenyekiti wa iliyokuwa Umoja wa Nchi Afrika (OAU), mwaka 1986 hadi 1987.

Kuporomoka kwa soko la mafuta katika miaka ya 1980, ilisababisha nchi hiyo kudorora kiuchumi.

Uchaguzi wa kwanza wa vyama vingi mwaka 1992, Sassou-Nguesso aliondolewa katika mzunguko wa kwanza na kumfanya Pascal Lissouba wa chama cha Pan-African Union for Social Development (Union Panafricaine pour la Démocratie Sociale; UPADS) kuteuliwa kuwania urais.

Sassou Nguesso, alianzisha siasa za vyama vingi mwaka 1990 na mwaka 1992 aliwania nafasi ya urais akashindwa, akaweka wa tatu.

Sassou Nguesso alikuwa kiongozi wa upinzani kwa miaka mitano, kabla ya kurejea madarakani wakati wa vita vya pili vya wenyewe kwa wenyewe mwaka 1997 hadi 1999.

Harakati hizo zilifanya vikosi vya waasi kumwondoa rais aliyekuwa madarakani, Pascal Lissouba.

**KATIBA ILIVYOMBEBA**

Kuanzishwa katiba mpya, kulikopitishwa na kura ya maoni mwaka 2015, kuliwezesha Sassou Nguesso, kusimama kwa muhula mwingine.

Akachaguliwa tena kuwania kiti cha urais wa mwaka 2016. Sassou Nguesso anaungwa mkono na vyama vingi vya siasa, muhimu zaidi ni PCT. Yeye ndiye Rais wa Kamati Kuu ya PCT.

***Makala hii imeandaliwa kwa msaada wa taarifa mbalimbali. Kesho usikose, makala kuhusu mpinzani wake aliyefariki kutokana na kuugua maradhi ya corona, siku ya uchaguzi, Machi 21, mwaka huu.***





# Majosho 129 kujengwa 2021/22

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

SERIKALI imesema kuwa katika mwaka wa fedha 2021/22 imepanga kuboresha sekta ya mifugo ikiwamo kujenga majosho 129, ili kuongeza thamani ya bidhaa zitokanazo na mazao ya mifugo.

Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, aliyasema hayo jana jijini Dodoma, wakati wizara yake ilipokuwa ikiwasilisha bajeti ya sekta ya mifugo kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Kilimo, Mifugo na Maji.

Alisema, wizara hiyo imejipanga kufanya maboresho makubwa katika sekta ya mifugo ili kuongeza thamani ya mazao yatokanayo na mifugo na kuchangia katika pato la taifa.

Ndaki alisema moja katika eneo ambalo watalifanyia kazi ni kujenga majosho 129, mapya pamoja na kukarabati yaliyopo ili kusaidia wafugaji kupata huduma hizo katika maeneo yao.

"Tutahakikisha kuwa tunajenga majosho kwa ajili ya kuogeshea mifugo kila eneo lenye mifugo nchini, lakini kukarabati majosho yote yalipo ili kuwezesha wafugaji kupata huduma za ugani katika maeneo yao," alisema.

Alisema, pia eneo jingine ambalo watalifanyia kazi ni kuboresha eneo la malisho kwa ajili ya mifugo ili kuwa na malisho ya uhakika na kupunguza migogoro baina ya wakulima na wafugaji.

"Katika hili sasa tumepunguza bei ya kukodisha maeneo ya malisho kwa kukodisha kwa Sh. 3,500 kwa heka kwa mfugaji atakaye hitaji eneo la malisho," alisema.

Vile vile, alisema kuwa katika mwaka huu wa fedha wamepanga kukusanya mapato katika sekta kiasi cha Sh. bilioni 50.

Awali akiwasilisha bajeti ya sekta ya mifugo mbele ya kamati hiyo, Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi anayesimamia sekta ya mifugo, Prof. Elisante Ole Gabriel, alisema itasaidia kuongeza thamani ya mifugo.

Alisema katika mipango ya bajeti ijayo wamepanga kuhakikisha kuwa wanawekeza katika kuboresha afya ya mifugo, pamoja na kutafuta masoko ya mazao ya mifugo.

"Katika kipindi hiki tutahakikisha kuwa tunatafuta masoko katika bidhaa za mazao ya mifugo kama vile nyama, ngozi, maziwa lakini kuongeza fursa nyingine ya matumizi ya vitu kama kwato, pembe na manyoya," alisema.

Aidha, alisema kuwa tayari wamepata wawekezaji kutoka nchi ya Slovakia, ambao wapenga kuja kuwekeza kiwanda cha kutengeneza mbolea kwa kutumia manyoya, pembe pamoja na kwato.

Hata hivyo, alitoa wito kwa wafugaji kutumia fursa ya mitamba ya kisasa iliyopo katika ranchi za taifa kufanya uhimilishaji ili kupata mifugo iliyobora itakayowasaidia kujikwamua kiuchumi na kuongeza pato la taifa.



Mpambe wa Rais akisindikizwa kuingia ukumbi wa Bunge, jijini Dodoma jana, alipofika kuwasilisha jina la Makamu wa Rais. PICHA: IBRAHIM JOSEPH

# Wanufaika wa TASAF wamkumbuka JPM

**Na Renatha Msungu, BAHI**

WANUFAIKA wa mpango wa kunusuru kaya maskini unaoratibiwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) wilayani Bahi mkoani Dodoma, wamesema hawatamsahau Hayati Dk. John Magufuli, kutokana na serikali yake kuwawezesha fedha wasichana wa umri wa kati na wanawake kwa ajili ya kujiinua kiuchumi.

Mpango wa kunusuru kaya maskini unalenga kuwasaidia fedha watu wasiojiweza kimaisha katika kaya maskini, ili kujikimu wao na famili zao.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti wakati wakielezea mafanikio waliyoyapata kutokana na fedha ambazo walipata kutoka TASAF, Lucy Ndoje alisema kupitia mradi wa timiza malengo ambao upo ndani ya mpango wa kunusuru kaya maskini wasichana na wanawake wengi wamejikwamua kwa kufanya ujasiriamali.

Ndoje alisema awali familia yake ilikuwa ikipata fedha kutoka TASAF ambazo waliweka akiba, huku yeye akabahatika kuingia kwenye kundi la wasichana waliobalee, ambao walipewa mitaji kwa ajili ya kuendesha biashara ambayo itamwezesha kujikwamua kiuchumi.

"Naishukuru serikali kupitia TASAF kubuni mradi wa timiza malengo kwa vijana na wanawake ulio ndani ya TASAF, ambao unalenga kusaidia jamii hiyo mitaji kwa ajili ya kuendesha biashara ambazo wamepanga kufanya," alisema Ndoje.

Naye Paulina Maine, ambaye anafanya biashara ya chakula, alisema baada ya kupata mtaji wa Sh. 160,000 kutoka TASAF alianza kuuza mchele na baadaye akaamua kufanya kazi ya mamalishe ambayo inamsaidia kuingiza kipato cha kujikimu yeye na familia yake.

Alisema mpango wa kunusuru kaya maskini umewasaidia kwa kiasi kikubwa watu wa rika zote kupanua wigo wa kufanya ujasiriamali kupitia fedha za mgao wa TASAF wanazoweka akiba.

"Tunaishukuru serikali kwa kuweka mpango huo, tunamuomba Rais Samia Suluhu Hassan aendeleze gurudumu hili ili wananchi kutoka kaya maskini wajikwamue kutoka walipo na kusonga mbele," alisema Maine.

Alisema wanaamini Rais Samia ataendelea kuwa mstari wa mbele kusaidia kaya maskini ili waweze kupiga hatua katika maendeleo ambayo wamekusudia kufanya.

Kwa upande wake, Jacqueline Kunze, alisema toka apate mtaji wa fedha za TASAF maisha yake na familia yake yamebadilika kwa kiasi kikubwa tofauti na ilivyokuwa awali.

Alisema yeye ni fundi nguo ambapo huwashonea watu nguo na kupata fedha kwa ajili ya kuendesha maisha yao ya kila siku.

"Natarajia kufika mbali katika ujasiriamali wa kushona nguo, nawashkuru TASAF kwa kunifikisha hapa nilipo," alisema Kunze.Kwa upande wake Ofisa Ufuatiliaji wa TASAF Wilaya ya Bahi, Christian Aman, alisema wasichana walioingia katika mradi wa Timiza Malengo wameweza kufanya mabadiliko makubwa katika familia zao kutokana na fedha ambazo waliwezeshwa kutumia kufanya ujasiriamali.

Alisema utekelezaji wa mpango wa TASAF awamu ya pili unaendelea, hivyo amewataka wananchi waliopo kwenye mpango huo kutumia nafasi hiyo kufanya ujasiriamali ambao unaleta matokeo chanya ndani ya jamii inayowazunguka.

# Serikali yaahidi upatikanaji wa dawa, vifaa tiba

**Na Paul Mabeja, DODOMA**

SERIKALI imesema itaendelea kuhakikisha upatikanaji wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi katika vituo vya kutolea huduma za afya unakuwa wa kuridhisha.

Hayo, yalielezwa juzi na Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, wakati akiwasilisha taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya wizara (Idara Kuu ya Afya) kwa kipindi cha Julai 2020 hadi Februari 2021 kwenye Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii jijini Dodoma.

Dk. Gwajima alisema katika kuhakikisha kuwa dawa zinapatikana kwa wakati na zenye ubora, serikali ilitenga kiasi cha Sh. bilioni 200, katika kipindi cha mwaka 2020/2021 kwa ajili ya ununuzi wa dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi.

Aidha, Dk. Gwajima alisema upatikanaji wa dawa katika vituo vya kutolea huduma za afya kwa aina 312 za dawa ambapo upatikanaji umefikia kiasi cha asilimia 74.

Hata hivyo, alisema wizara imeboresha huduma za afya ya uzazi katika kipindi cha Julai 2020 hadi Februari 2021, ambapo jumla ya wajawazito 1,165,526 sawa na asilimia 103 ya waliotarajiwa walihudhuria kliniki na kupata huduma.

"Kati ya wajawazito hao asilimia 36.5 ndio walianza huduma kabla ya wiki 12, ikilinganishwa na asilimia 36.4 kipindi kama hiki mwaka 2019," alisema.

Aliongeza kuwa asilimia 90.4 walifanya mahudhurio manne au zaidi ikilinganishwa na asilimia 84.1 mwaka 2019.

Kwa upande wa waliojifungulia katika vituo vya kutolea huduma za afya, Dk. Gwajima alisema wajawazito 920,126 sawa na asilimia 82 kama ilivyokuwa katika kipindi kama hicho mwaka 2019.

Alisema katika kuimarisha huduma za kinga hususani huduma za chanjo, jumla ya watoto wa chini ya mwaka mmoja 1,030,617 walitarajiwa kupatiwa chanjo kwa ajili ya kuwakinga na magonjwa mbalimbali na hadi kufikia Februari 2021 watoto 1,010,005 sawa na asilimia 98 walipatiwa chanjo kwa kutumia kigezo cha PENTA-3 kwa mujibu wa mwongozo wa Shirika la Afya Duniani (WHO).

**Aliongeza kuwa asilimia 90.4 walifanya mahudhurio manne au zaidi ikilinganishwa na asilimia 84.1 mwaka 2019**





# Shirika lapongezwa kuwaandaa wanawake kiuongozi

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

VITUO vya taarifa na maarifa kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya na Same mkoani Kilimanjaro, vimepongeza Shirika lisilokuwa la kiserikali la TGNP- Mtandao kwa kuwaandaa wanawake kushiriki na kuwa viongozi wa ngazi mbalimbali.

Wakizungumza jana kwenye kikao cha kubadilishana uzoefu wa mafanikio waliyoyapata wanawake wa vituo vya taarifa na maarifa kutoka wilaya za Mbeya na Same ambacho kinafanyika jijini Mbeya, wanawake hao wamesema TGNP- Mtandao wamewaandaa vya kutosha kuwa viongozi.

Mwenyekiti wa Kituo cha Taarifa na Maarifa Kata ya Nsalala, wilayani Mbarali, Felister Kaisi, alisema hadi sasa wanajivunia kupata mafanikio mengi baada ya kujengewa uwezo na TGNP-

Mtandao katika masuala ya uongozi, ukatili wa kijinsia na kuhamasisha shughuli za maendeleo katika jamii.

Kutokana na mafanikio hayo ya kujengewa uwezo kuwa viongozi, Felister alisema jumla ya wanawake wanne kati ya saba waliogombea walishinda kwenye nafasi ya uenyeviti wa vitongoji kwenye uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka 2019.

Alisema viongozi hao ni wachapa kazi wanaoshughulikia matatizo ya wananchi ikilinganishwa na dhana iliyokuwapo kwamba hawataweza kuwa viongozi bora.

"Jamii imebadili mtazamo hasi kuhusu wanawake ambao walikuwa wanakandamizwa na mifumo dume, kukosa haki ya kumiliki ardhi, unyanyasaji wa kingono na vipigo, matunda hayo ni kutokana na jitihada za TGNP- Mtandao kuwajengea uwezo wananchi hususani waishio pembezoni kupaza sauti zao, lakini pia kuwawezesha kutoa elimu ili kukabiliana na vikwazo hivyo," alisema Felister.

Pia wamejenga imani kwa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya kushirikishwa kwenye shughuli mbalimbali za maendeleo ikiwamo ushiriki wa vikao vya Baraza la Madiwani kutoa mapendekezo ya bajeti inayozingatia mlengo wa kijinsia.

Kwa upande wake, Happiness Mhina, kutoka Kata ya Lugulu, wilayani Same, Mkoa wa Kilimanjaro, alisema TGNP- Mtandao imewajengea uwezo wa kuwa viongozi bora na majasiri.

Alisema elimu hiyo ilimshawishi na yeye kugombea nafasi za udiwani kwenye kata yake ya Lugulu mwaka 2020, lakini kura za maoni hazikutosha na bado nia yake ni kuwa kiongozi.

Kadhalika, vituo vya taarifa na maarifa nchini vinaendelea kumwombea afya njema Rais wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan, kuendelea kuwatumikia wananchi kwa uzalendo na moyo wa ushujaa kama ilivyo sasa.

Alisema rais huyo ni mfano wa kuigwa kwa sababu amekuwa mtulivu, mwenye busara anayetatua mambo kwa utashi mkubwa.

Sabina Mwalyego kutoka Kata ya Mshewe, wilayani Mbeya, alisema wamesaidia kutatua vikwazo mbalimbali vinavyowakabili wananchi, ikiwamo suala la maji, afya, elimu, kilimo na utawala bora.

Alisema wamekuwa wahamasishaji wa shughuli za maendeleo kwa kuwaelimisha wananchi kushiriki, lakini kupaza sauti zao ya vikwazo wanavyokabiliana navyo.

Amina Juma, mkazi wa Kata ya Kalemawe, wilayani Same alisema, pia wamepata elimu ya ujasirimali.

Alisema kwa sasa wana mashine ya kutengeneza taulo za kike, mradi ambao umewasaidia kujikwamua kiuchumi na kuwasaidia watoto kujisitiri.



Mwenyekiti wa Vituo vya Taarifa na Maarifa, Kata ya Nsalala, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Felister Kaisi (kushoto), akimkabidhi nakala ya kitabu kinachohusu masuala ya wanawake na uongozi Happiness Mhina wa Kata ya Lugulu wilayani Same mkoani Kilimanjaro, wakati wa kikao cha kushirikishana na kujadiliana mafanikio waliyoyapata baada ya kujengewa uwezo na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), jijini Mbeya juzi. PICHA: GRACE MWAKALINGA

# 'Hayati Magufuli alitufundisha nidhamu ya fedha'

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

VIONGOZI wa mila katika Wilaya ya Mbarali, mkoani Mbeya, wamesema utawala wa aliyekuwa Rais wa Tanzania, Hayati Dk. John Magufuli uliwafundisha Watanzania kuwa na nidhamu ya matumizi ya fedha ambayo imesaidia kuinua uchumi wao na kuepusha migogoro ya kijamii.

Viongozi hao kabila la Wasangu waliyasema hayo, wakati wa ibada ya kumwombea heri aliyekuwa Rais wa Tanzania, Hayati Dk. Magufuli, ambayo yaliandaliwa na Chama Cha Mapinduzi Wilaya ya Mbarali na kuwakutanisha wananchi bila kujali tofauti za imani zao ambayo imefanyika katika mji mdogo wa Rujewa.

Katibu wa mila wilayani humo, Mwanasimtwa Mwagongo, alisema Hayati Dk. Magufuli, aliwaonyesha njia na kuwafundisha watu adabu na kuwaonyesha matumizi sahihi ya fedha ili kufikia malengo waliyojiwekea.

Alisema aliwafundisha wanaume kuacha michepuko na kuwa na mke mmoja kwa maana fedha zilikuwa ngumu kupatikana na iliyokuwa inapatikana iliheshimiwa na kuelekezwa kwenye matumizi sahihi.

"Uongozi wa Hayati Dk. Magufuli ulikuwa darasa kwetu kwani alitufundisha uzalendo kuheshimu matumizi ya fedha kwa kuelekeza maeneo muhimu, wanaume kuacha michepuko na watu kuokoka ili kupunguza au kuacha anasa, tutaendelea kumwombea apumzike kwa amani," alisema Mwagongo.

Mwenyekiti wa CCM, Mbarali, Hashim Mwalyao, alisema watasimamia mambo yote aliyoasisi Hayati Magufuli kwa ajili ya maendeleo ya taifa.

Alisema chama kitaendelea kukagua miradi mbalimbali ya maendeleo ili fedha zilizotumika ziendane na uhalisia wa miradi inayojengwa au kukamilika.

Mbunge wa Jimbo la Mbarali, Francis Mtega, alisema, walifundishwa kuchapa kazi ili kumudu gharama za maisha na kulisaidia taifa kutokuwa tegemezi.

Mkuu wa wilaya hiyo, Reuben Mfune, aliwaonya watu wanaodhani serikali itayumba kutokana na kifo cha Hayati Magufuli na badala yake alisema viongozi waliopo wataendelea kuchapa kazi kwa bidii ili kufikia malengo yaliyokuwa yakitarajiwa.

# Baadhi kinamama huchangia utapiamlo kwa watoto

**Na Grace Mwakalinga, MBEYA**

BAADHI ya wanawake mkoani Mbeya, wanadaiwa kuchangia tatizo la utapiamlo kwa watoto kutokana na kushindwa kufuata ushauri wa wataalamu wa afya namna ya kunyonyesha.

Hayo yalisemwa hivi karibuni na Ofisa Lishe, Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mbeya, Dk. Charles Msigwa, alieleza kuwa mtoto asiponyonyeshwa maziwa ya mama kwa kipindi cha miezi sita ya mwanzo ana hatari kubwa ya kukosa virutubisho muhimu vinavyohitajika kwa ajili ya ukuaji wake na kusababisha utapiamlo.

Alisema baadhi ya watoto wanaopimwa kliniki katika hospitali hiyo afya zao sio za kuridhisha, kutokana na wengine kudhoofu na wengine kuwa na tumbo kubwa.

Alisema miongoni mwa sababu zinazosababisha utapiamlo kwa watoto ni kinamama wengi kuwa bize na shughuli mbalimbali za uzalishaji na ujasiriamali ambao hushindwa kumaliza miezi sita wakihofia kukwamisha kazi zao.

"Mtoto asiponyonyeshwa kwa miezi sita ya mwanzo anaweza kupata ugonjwa wa kwashakoo au utapiamlo, tumejitahidi kutoa elimu ya unyonyeshaji kwa kinamama, lakini wengine hawazingatii matokeo yake watoto wanapata maradhi," alisema Msigwa.

Dk. Msigwa alisema zipo athari zitokanazo na mama kutomnyonyesha mtoto ikiwamo saratani ya matiti kwa sababu maziwa yanayotakiwa kutoka yanaganda ndani na kutengeneza mafuta.

Mmoja wa wanawake kutoka Mtaa wa Juhudi jijini humo, Jenifer Kabuka, alisema kinachosababisha kuwaachisha maziwa watoto ni hali ngumu ya maisha na hulazimika kwenda mashambani au kufanya shughuli za ujasiriamali ili kupata fedha za kuendesha maisha yao.

Jenifer alisema kwa sababu ya kuwa na kazi nyingi na shughuli za kujiingizia kipato, watoto hunyweshwa uji ili asisumbue.

## Z'bar yathamini mchango Chuo cha Ushirika Moshi

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

OFISI ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji Zanzibar, imesema inathamini mchango na juhudi zinatolewa na Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi, kuimarisha sekta ya ushirika nchini.Mkurugenzi wa Idara ya Uendeshaji na Utumishi, January Fusi, alisema hayo kwa niaba ya Katibu Mkuu, alipokuwa na mazungumzo kati ya uongozi wa wizara na Mkurugenzi kitengo cha kuendeleza elimu ya ushirika kutoka Chuo Kikuu cha Ushirika, Dk. Gervas Machimu, Mwanakwerekwe Zanzibar.

Alisema Zanzibar ni wadau wazuri na elimu inayotolewa na chuo hicho imesaidia sekta hiyo kufanya vizuri na wananchi kupata mwamko kwa kuanzisha vyama vingi vya ushirika mjini na vijijini.Alisema wananchi wamejiajiri na kuajiriwa kupitia sekta ya ushirika na kusaidia serikali kupunguza tatizo la ajira.

Aliushukuru uongozi wa chuo hicho kwa kuendeleza ushirikiano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na ni jambo la kuendeleza.

Naye Mkurugenzi wa kitengo cha kuendeleza elimu ya ushirika, Dk. Gervas Machimu, aliyemwakilisha Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi, alisema amefurahishwa kuona mrejesho wa taaluma wanayoitoa Zanzibar hatua inayowapa msukumo wa kuendeleza ushirikiano wa kutoa elimu kuhusu ushirika.Alisema maofisa ushirika wanafanyakazi vizuri na kwa weledi na idara ya ushirika imewapokea na inashirikiana nao vizuri.

"Tumekuja na rasimu ya maridhiano ya ushirikiano ya miaka mitano na tunashauri kuwapo chombo kitachosimamia mpango huo, hii itasaidia kuona tunafikia malengo tuliyojipangia na kusaidia kujenga umoja wa kitaifa," alisema.

Alisema kupitia ushirikiano huo wanaweza kuratibu na kutoa elimu kupitia programu mbalimbali kuanzia ngazi ya chini hadi chuo cha ushirika wanaweza kuandaa programu za pamoja itasaidia kuratibu sekta hiyo.Aliyataja maeneo ya ushirikiano kuwa ni pamoja na kuibua miradi, kujengewa uwezo wanaushirika, kuendeleza biashara ya ushirika na kuandaa makala kwa pamoja.

# Sekta elimu kuendelezwa kuongeza kiwango cha ufaulu

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

WAZIRI wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Simai Mohammed Said, amesema atahakikisha anashirikiana na kila mdau wa elimu ili sekta hiyo inaendelea kupiga hatua kwa kuongeza kiwango cha ufaulu kwa wanafunzi.

Alisema kumekuwapo na matatizo mengi kwa walimu hasa waliotumikia muda mrefu kazini na kusababisha kupungua kwa ufanisi katika utendaji wa kazi zao.

Aliyasema hayo jana katika mkutano na walimu wenye matatizo ya maradhi mbalimbali pamoja na wanaokaribia kustaafu kazi, kwa Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja.Alisema atahahakisha matatizo yao yanafanyiwa kazi hatua kwa hatua ili kuleta mabadiliko katika maeneo mbalimbali ya sekta hiyo.

Alisema ni changamoto kubwa kwa walimu kupata matatizo ya kiafya na baadhi yao ni kutokana na miundombinu chakavu ilioko katika shule pamoja na vifaa wanavyofanyia kazi.

Alisema mapinduzi ya kielimu yanahitaji mkazo wa kila mtu, aliwataka walimu hao kuendelea kuwa na uvumilivu huku matatizo pamoja na madai yao yakiendelea kufanyiwa kazi.

Alisema lengo la Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ni kuboresha huduma kwa wananchi wake kwa kuhakikisha upatikanaji wa elimu bora unaimarika zaidi nchini kote.

Akizungumzia suala la kuanzisha tume maalum ya utumishi kwa walimu, alisema bado linaendelea kufanyiwa kazi ili kulitatua kwa haraka baadhi ya changamoto zinazowakwaza walimu hao.

Kuhusu suala la udhalilishaji, Waziri Simai alisema walimu wana nafasi kubwa kushirikiana na wazazi kuhakikisha wanamaliza vitendo hivyo katika jamii na sio kuendelea kuhusishwa kwa sababu vitendo hivyo vimekuwa vikitia doa kazi yao.

Kwa upande wao walimu hao, waliomba wizara kuboresha baadhi ya miundombinu iliyochakaa katika shule pamoja na kuboresha mifumo ya utumiaji wa chaki ambayo husababisha kupata madhara mbalimbali ya kiafya na kusababisha kutofanya kazi zao vizuri.

Pia waliiomba Wizara ya Elimu Zanzibar, kuwaanzishia mfumo wa matumizi ya bima ya afya watendaji wake ili kupunguza usumbufu wanapohitaji matibabu ya haraka.



Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Simai Mohammed Said, akinawa mikono alipofika katika Shule ya Sekondari Kiembe Samaki kwa ajili ya kuzungumza na walimu, jana. PICHA: RAHMA SULEIMAN

# Asasi zajenga matumaini kwa Samia

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

UMOJA wa Asasi za kiraia Zanzibar umesema umejenga matumaini makubwa ya kufanya kazi na Rais wa Tanzania Samia Suluhu Hassan, katika kuzipatia ufumbuzi changamoto zinazolikabili taifa kwa lengo la kupiga hatua kubwa kimaendeleo.

Wakitoa taarifa kwa waandishi wa habari, Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Asasi za Kiraia (ANGOZA), Hassan Khamis, alisema Rais Samia wanamfahamu kiutendaji na uzoefu na uwezo wake wa kufanya kazi katika sehemu mbili za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ikiwamo Zanzibar na Tanzania Bara.

Alisema Watanzania wameondokewa na aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano, Dk. John Magufuli, lakini matarajio makubwa ni mambo muhimu ya maendeleo yaliyotekelezwa katika kipindi hicho yatasimamiwa vizuri na Rais Samia.

Aliyataja baadhi ya mambo hayo muhimu ikiwamo miradi ya kimkakati iliyoasisiwa na Hayati Rais Magufuli ni mradi wa kuzalisha umeme wa Mto Rufiji Stigler Gauge ambao utaiwezesha Tanzania kuzalisha umeme megawati 2115.

Pia alisema elimu bure ya ngazi ya msingi kwa wanafunzi wote ikiwamo wa wazazi maskini kuendelea kutolewa kwa sababu imewasaidia kwa kiasi kikubwa wazazi ambao wengi wao walikuwa wakiishi katika maisha magumu ya kushindwa kumudu kulipa ada ya shule ya kila mwaka.

"Hayo ni baadhi ya mambo muhimu yaliyofanywa na Rais Magufuli katika kipindi cha uongozi wake wa miaka mitano... matarajio yetu makubwa kwamba yataendelezwa katika kipindi cha uongozi wa Rais Samia," alisema.

Khamis alisema wanafahamu uwezo mkubwa wa uongozi alionao Rais Samia ambaye kabla ya kuingia katika siasa alipata kufanyakazi katika Shirika la Muungano wa Asasi za kiraia (ANGOZA).

Alisema katika kipindi hicho alishiriki katika mijadala na makongamano mbalimbali na kwamba kusaidia kuimarika kwa uhai wa asasi hizo na kuwa miongoni mwa watetezi wakubwa wa demokrasia pamoja na maendeleo ya sekta mbalimbali.

Mkurugenzi wa asasi za kiraia ya ZAFAICO, Abdalla Abeid, alisema matarajio ya asasi nyingi ni kufanya kazi kwa karibu sana na Rais Samia kuona asasi zinatimiza majukumu yake ya kuanzishwa kwa mujibu wa sheria.

Alisema asasi za kiraia zitafanya kazi kwa karibu na Rais Samia katika kuimarisha utawala bora, uwajibikaji na kuleta ufanisi kwa kutoa elimu kwa wananchi katika kujenga nchi yao kwa kuzingatia vigezo vya uzalendo.

Jumla ya asasi 12 zilizopo Unguja na Pemba zimeshiriki kutoa tamko la kumuunga mkono Rais Samia kikiwamo Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake (TAMWA) Zanzibar, Jumuiya ya Waandishi wa Habari za Maendeleo (WAHAMAZA), Jumuiya ya Wanasheria Zanzibar (ZLS) na Muungano wa asasi za kiraia ANGOZA.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**Uza,**
**Chenye Thamani Kubwa**
**Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa**
**Tupigie 0782253676**

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.7**
**2021**
**In the matter of the Estate of the late NICKSON NICHOLAUS KANO of Kikuyu Area within Dodoma Region**
**AND**
**IN THE MATTER OF THE APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION BY ERASTO JOSEPH KANO**
**GENERAL CITATION**
**(RULE 75 OF PROBATE RULES GN 369 OF 1963)**

**ALL PERSONS** claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 6th Day of **APRIL 2021**
Date at Dodoma this 24th Day of February 2021
**Presented for filing this 12 day of 3 2021**

RESIDENT MAGISTRATE

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

Ndugu **GWAMAKA J MSSIKA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA SUCCEED WAGON** yenye namba za usajili **T 885 DQT**. Yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
Polisi taarifa
**KAS/RB/3003/2020**

## KUPOTELEWA KWA KADI YA GARI

**HERITAGE MICROFINANCE** inatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T156 ATJ Nissan Pathfinder.** Chasses namba **JNIVA2R50A000384** Engine namba **VG33029325** . Model namba **JNB4D** ya mwaka 1998
Atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.
Taarifa ya polisi :
**ARU/THE/RB/34296/2021**

## TANGAZO LA KUFUNGA KAMPUNI

WAMILIKI WA KAMPUNI YA MEDALLION LIMITED (NAMBA YA USAJILI 142-132-419 YA TAREHE 14 JULY 2020) WANAPENDA KUUTANGAZIA UMMA KUWA KAMPUNI YAO IMESITISHA BIASHARA ZAKE NA HIVYO KUAMUA KUIFUNGA KWA MUJIBU WA SHERIA YA MAKAMPUNI BRELA.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**FORM II**
**(S.M.M. 1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

Katika Mahakama ya Mwanzo **– KIMARA**
Usimamizi wa mirathi **No. 55/2021**
Ombi la **POLLYN REMMY MSOFE** kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu **GASPER REMMY MSOFE**
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe **5/4/2021** kabla ya huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia wa marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa.

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA DAR ES SALAAM**
**SHAURI LA MADAI NA.193 YA 2019**
**BURAK BUYUKSARAC MDAI**
**DHIDI YA**
**TPM MINING AND ENERGY LIMITED MDAIWA**
**TPM MINING AND ENERGY LTD,**
**P O BOX 89006,**
**DAR ES SALAAM**
**KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa aliyetajwa hapo juu,ameleta shauri la maombi ya madai dhidi yako,maombi ambayo maelezo yake yameelezwa katika nakala za maombi ya madai ambazo zinapatikana katika mahakama hii.hivyo basi unahitajika kuhudhuria katika mahakama hii kupitia wakili au mwakilishi wako ambaye anaruhusu kisheria siku ya tarehe 6 may 2021 saa tatu 3:00 kamili asubhi mbele yam he.R.A.EBRAHIM,-JUDGE kujibu maombi hayo dhidi yako.
Unaagizwa kuleta vielelezo vyote ambavyo unatarajia kuvitumia kwaajili ya utetezi siku hiyo.
ANGALIZO.
Kama usipohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na mahakama ikithibitisha kuwa umepokea taarifa hii ya kuitwa shaurini,basi shauri linaweza kusikilizwa na kuamuliwa bila uwepo wako.
Hati hii imetolewa kwa AMRI yangu na chapa ya mahakama hii leo tarehe 18 mwezi march 2021

DEPUTY REGISTRAR
DAR ES SALAAM ZONE

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

NEEMA SALEHE JOSEPH ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI T 797 DTH AINA YA TOYOTA BREVIS.
KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI.
TAARIFA YA POLISI:
KAH/TR/RB/140//2021

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**IBRAHIM KATANI NYANDA** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya bajaji yenye namba za usajili **T. 979 CXM**, yenye Chases no. **10525194**, Engine no. **78611291**.Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo karibu yake. Taarifa ya Polisi.
**MWA/NY/ RB/131967 /2021.**

Kwa Habari
Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
MWANGA WA JAMII

OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## TANGAZO



# SALAMU ZA PONGEZI

Uongozi na Wafanyakazi wa Makampuni ya IPP unakupongeza Dkt. Philip Isdor Mpango kwa kuteuliwa kuwa Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Tunakutakia kheri katika majukumu yako mapya.

IPP



# LIVERPOOL

## WAJITOSA KUMSAJILI KONATE

**LIVERPOOL, England**

LIVERPOOL imeripotiwa kuwa ipo kwenye hatua kubwa zaidi ya mazungumzo juu ya dili la uhamisho wa beki wa kati wa RB Leipzig, Ibrahima Konate.

Liverpool waliwasogeza Ozan Kabak na Ben Davies kwenye usajili wa Januari ili kuziba mapengo ya Joe Gomez na Virgil van Dijk waliopata changamoto ya majeraha.

Licha ya kuwa na ongezeko la nafasi za ulinzi kwa dirisha la Januari, kocha Jurgen Klopp anaaminiwa kuwa yupo katika mchakato wa kumleta mlinzi mwingine klabuni hapo kuelekea msimu ujao.

Konate, ambaye anatajwa kuwa na uwezo wa kucheza pia beki ya kulia na winga ya kulia, ndiye mchezaji anayetajwa zaidi kuwapo kwenye orodha ya wachezaji anaowataka Klopp.

Kwa mujibu wa gazeti la The Athletic, mabosi wa Liverpool wamekuwa wakifanyia kazi suala hili nyuma ya pazia kuhakikisha linaenda sawa, na wako mbioni kukubaliana na Leipzig dili la ada ya paundi milioni 40. Chelsea pia wanatajwa kuwa wapinzani wa Liverpool kuinasa saini hiyo.

# INTER KUKAMILISHA MALIPO YA HAKIMI

**MILAN, Italia**

INTER Milan inatarajia kulipa ada ya paundi milioni 13 kwa ajili ya nyota Achraf Hakimi kwa Real Madrid, kama sehemu ya usajili wao wa mwaka 2020.

Nyota huyo raia wa Morocco, aliungana na kikosi hicho cha Antonio Conte mwanzoni mwa msimu huu kwa dili lililotajwa kuwa na thamani ya paundi milioni 40.


Thamani ya dili hili lilikuwa linategemea kiwango atakachokionyesha nyota huyo katika mafanikio yake kwenye Ligi Kuu Italia, Serie A, akiwa na kikosi cha Conte ambacho kwa sasa kinaongoza msimamo wa ligi hiyo.

Kwa mujibu wa Gazzetta dello Sport, kupitia Mundo Deportivo, Inter sasa watalipa ada iliyokubaliwa kukamilisha dili la awali.

Klabu zilikubaliana malipo ambayo yalipaswa kukamilishwa mwisho wa mwaka uliopita na yanatakiwa kukamilishwa Machi 2021, ili kuendana na mwongozo wa UEFA wa masuala ya fedha kabla ya mwisho wa mwaka wa fedha.

Hakimi ameweza kuendana haraka na hali ya Serie A na kuwa sehemu muhimu ya mipango ya Antonio Conte, akiwa amecheza mechi 26 za ligi na mabao sita kwa msimu huu wakitarajia kumaliza ukame wa taji wa miaka 11 pale San Siro.

# IBRAHIMOVIC: SINA KITU ZAIDI CHA KUTHIBITISHA



**STOKHOLM, Sweden**

STRAIKA wa AC Milan, Zlatan Ibrahimovic, aliwasaidia Sweden kuwatandika Kosovo na kusema kuwa anatambua kuwa si wengi wanaoweza kufanya kile anachokifanya yeye wakiwa na umri wa miaka 39.

Sweden walishinda bao 1-0 kabla ya kupata ushindi mwingine wa mabao 3-0 dhidi ya Kosovo kwenye hatua ya kufuzu Kombe la Dunia.

"Sina kitu zaidi cha kuthibitisha", alisema Ibrahimovic ambaye amerejea kwenye timu ya taifa wiki iliyopita kwenye mechi dhidi ya Georgia.

Nyota huyo ambaye ameweka wazi kuwa hali yake sasa imebadilika linapokuja suala la soka, na kwake hiki ni kipindi cha kufurahia tu katika maisha yake ya soka kutokana na kile anachokifanya.

"Sasa nipo katika hali tofauti kabisa," aliongeza.

"Kwa sasa sina kitu kilichosalia cha kuthibitisha, hakuna kitu kipya cha kufanya kwenye soka langu la kulipwa zaidi ya kufurahia tu.

"Ninamaanisha kuwa nina miaka 39, na ninacheza timu ya taifa si wengi wanaweza kufanya hivyo wakina umri kama wangu."

## HABARI MICHEZO



# MWAMUZI

## AOMBA RADHI KUKATAA BAO LA RONALDO

**AMSTERDAM, Uholanzi**

MWAMUZI Danny Makkelie ameomba msamaha kwa Cristiano Ronaldo na Ureno baada ya kukataa bao la mshambuliaji huyo dhidi ya Serbia.

Ureno ililazimishwa sare ya 2-2 katika mechi hiyo ya kuwania kufuzu Kombe la Dunia 2022 nchini Qatar, baada ya Ronaldo bao lake kukataliwa.

Baada ya marudio ilionyesha kwamba, shuti la mshambuliaji huyo wa Juventus lilikuwa limevuka mstari kabla Aleksandar Mitrovic kuuondoa mpira huo.

Lakini mwamuzi Makkelie ambaye ni raia wa Uholanzi, aliruhusu mpira kuendelea baada ya kushauriana na wasaidizi wake, ambaye sasa amekiri kuwa ulikuwa ni uamuzi mbaya.

"Kwa mujibu wa kanuni za Shirikisho la Soka la Kimataifa (Fifa), ninachoweza kusema ni kwamba niliomba msamaha kwa kocha wa timu ya Taifa ya Ureno, Fernando Santos, kwa kile kilichotokea," alisema Makkelie akiliambia gazeti la A Bola la nchini Ureno.

"Kama timu ya waamuzi, kila wakati tunafanya bidii kufanya maamuzi mazuri. Tunapokuwa kwenye habari kwa njia hii, haitufurahishi hata kidogo."

Ronaldo alikasirika baada ya kuona bao lake limekataliwa, baada ya kumalizia pasi ya Nuno Mendes iliyoingia langoni kabisa.

Zilikuwa zimebaki sekunde chache mchezo huo kumalizika na Ronaldo alikataa kuendelea na mchezo na akakitupa kitambaa cha unahodha na kutoka nje ya uwanja.

Ronaldo alitupa kitambaa chake chini, na akaelezea majibu yake kwenye mitandao yake ya kijamii baada ya mchezo.

"Daima nitajitoa kila kitu kwa nchi yangu, hiyo haitabadilika kamwe," alisema kwenye Instagram.

"Lakini kuna nyakati ngumu kushughulika nazo, haswa wakati tunahisi kuwa taifa zima linaumizwa."

## MULLER ATANGAZA KUONDOKA BAYERN

**MUNICHA, Ujerumani**

THOMAS Muller amekiri kwamba, yupo tayari kufuata nyayo za Thiago Alcantara kwa kuondoka pale kwenye dimba la Allianz Arena na kusisitiza "sijazuiwa" na Bayern Munich.

Muller alianza kucheza soka la kulipwa Bayern Munich mwaka 2008 na tangu kipindi hicho ameisaidia klabu hiyo kupata mafanikio makubwa ndani ya Ujerumani na katika Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31, bado amesalia kuwa ni mchezaji muhimu ndani ya kikosi hicho, lakini ni kama anaonekana kukaribia kufanya maamuzi kama Thiago alivyohamia Liverpool mwaka 2020 na kudhihirisha kuwa hakuna mtu ambaye hawezi kuondoka klabuni.

"Sijafungwa katika klabu hii," alisema mshambuliaji huyo wa Bayern akiliambia gazeti la Times.

"Nina uhusiano maalumu, ninaipenda Bayern Munich kabla hata sijaanza kuichezea, lakini kama kuna hali inayokusababisha kufanya maamuzi labda ya kwenda klabu nyingine, unafanya na haitakuwa aibu wala haitakuwa tatizo."

Muller amecheza michezo 571 katika mashindano yote kwa Bayern Munich na amefanikiwa kufunga mabao 212 na kutoa pasi za mwisho 210.

Mshambuliaji huyo amefanikiwa kushinda mataji 27 makubwa, tisa ya Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, na mawili ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Mkataba wa sasa wa Muller unatarajiwa kumalizika mwaka 2023 na kocha Hansi Flick amekuwa akimwamini sana katika kuongoza kikosi akisaidiana na Robert Lewandowski.




## MBAPPE NUSURA ATUE DOTMUND

**DORTMUND, Ujerumani**

SKAUTI wa wachezaji wa zamani wa Borussia Dortmund, Sven Mislintat, amefichua kwamba, Borussia Dortmund walikuwa wamekaribia kumsajili, Kylian Mbappe kwa uhamisho wa bure mwaka 2016.

Mbappe amekuwa mmoja wa wachezaji bora baada ya kuonyesha kipaji chake na baada ya kucheza mechi yake ya kwanza kule Monaco mwaka 2015.

Alipomaliza msimu wake wa kwanza pale katika dimba la Louis II klabu zote kubwa zilianza kuonyesha nia ya kumhitaji raia huyo wa Ufaransa, na Mislitant amedai kwamba, Dortmund ilikuwa karibu sana kumnasa mchezaji huyo.

Skauti huyo ameliambia jarida la Kicker jinsi alivyoshindwa kumpeleka Mbappe pale Westfalenstadion: "Ilikuwa ni aibu kwamba, tumeshindwa kumpata Mbappe."

"Kylian Mbappe alikuwa anapatikana bila malipo ingawa, klabu nyingi zilikuwa zikivutiwa naye, lakini tulishindwa kufanikisha dili.

"Kama tungeweza kumpata Mbappe kutoka Monaco kwa uhamisho huru kwa wakati ule, ingekuwa dili kubwa sana."

Lakini Paris Saint-Germain ndio iliyofanikiwa kumsajili Mbappe kwa dili lenye thamani ya euro milioni 180 na kumfanya kuwa mchezaji kinda ghari zaidi katika historia.

Mbappe atarudi dimbani kwa Paris Saint-Germain pale watakapokabiliana na Lille Aprili 3, mwaka huu, katika Ligue 1.

## HABARI MICHEZO

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# AGUERO AGEUKA LULU BARCA, JUVE NA PSG

●●●Licha ya kuripotiwa angependa kurejea nyumbani kwake nchini Argentina katika klabu ya utotoni, lakini...

**MANCHESTER, England**

MSHAMBULIAJI wa Manchester City, Sergio Aguero ameripotiwa kugombewa na Barcelona, Juventus na Paris Saint-Germain, ambao wanatajwa kuiwinda saini yake.

Mchezaji huyo wa zamani wa Atletico Madrid, anatarajia kumaliza muda wake pale Etihad mwishoni mwa msimu huu na licha ya umri wake kuonekana kumtupa mkono na changamoto za majeruhi, bado hatarajiwi kuwa mchezaji wa kukosa timu ya kwenda.

Aguero mwenye umri wa miaka 32, ameripotiwa kuwa angependa kurejea nyumbani kwake nchini Argentina katika klabu ya utotoni Independiente del Valle, lakini klabu hizo tatu za Ulaya zinaamini kuwa anaweza kuwatumikia vema. Kwa mujibu wa Marca, PSG, Juventus na Barcelona zote zinatajwa kuwa na matarajio ya kumnasa nyota huyo kwa uhamisho huru kipindi cha majira ya joto.

Barca wakiwa na matumaini kuwa kuwasili kwa mshambuliaji huyo kunaweza kumshawishi Lionel Messi kutia saini mkataba mpya, maana ni rafiki yake mkubwa.

Baada ya Juve kutupwa nje kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya na Porto, ripoti tofauti ilionyesha kwamba 'Kibibi Kizee' hicho cha Italia kinataka kumsajili Aguero ili kumthibitishia Cristiano Ronaldo kwamba, wanaunda kikosi chenye uwezo wa kutawala Ulaya.

Msimu huu umekuwa mgumu kwa Aguero akipata changamoto ya majeraha, akilazimika kucheza mechi 14 tu kwenye michuano yote na kuona lango mara mbili.

## KWA UFUPI

**BECKHAM AMTAKA STURRIDGE**

MMILIKI wa Klabu ya Inter Miami ya Marekani, David Beckham, ambaye kocha wake ni Phil Neville, imesimama imara dhidi ya mahasimu wao katika Ligi Kuu Marekani ya Major League DC United kwenye kinyang'anyiro cha kumsajili aliyekuwa mshambuliaji wa England, Liverpool na Chelsea, Daniel Sturridge mwenye umri wa miaka 31, ambaye amekuwa huru tangu alipoondoka klabu ya Uturuki ya Trabzonspor Machi, 2020. ***(Mirror)***

**LIVERPOOL KUMFUNGA WIJNALDUM**

BARCELONA imetoa mkataba wa miaka mitatu kwa kiungo wa kati wa Liverpool, Georginio Wijnaldum mwenye umri wa miaka 30, ambaye atakuwa huru mwishoni mwa msimu huu. ***(Mundo Deportivo)***

**SABITZER AWANIWA UNITED**

KLABU za Manchester United, Liverpool na Tottenham zinawania kumsajili kiungo wa kati wa Austria, Marcel Sabitzer mwenye umri wa miaka 27, kutoka RB Leipzig. ***(Bild, via Sun)***

**EVERTON KUMUUZA MINA**

EVERTON ipo tayari kupokea ofa kwa wanaotaka kumsajili mlinzi wa Colombia mwenye umri wa miaka 26, Yerry Mina. ***(Football Insider)***

**ALABA AWANIWA CHELSEA, PSG**

CHELSEA na Paris St-Germain zimetajwa kama timu ambazo kuna uwezekano mkubwa mlinzi wa Austria, David Alaba mwenye umri wa miaka 28, anaweza kujiunga nazo, baada ya wakala wake, Pini Zahavi kupuuza uvumi kuwa ni Real Madrid na Barcelona pekee ndizo zinazomnyatia mchezaji huyo. ***(Diario AS, via Mail)***

**MENINO AGOMBEWA ULAYA**

JUVENTUS imejiunga na Tottenham, Chelsea na Atletico Madrid kumsaka kiungo wa kati wa Brazil, Gabriel Menino mwenye umri wa miaka 20, ambaye huenda akaruhusiwa kuondoka Palmeiras kwa pauni milioni 13 kwa sababu ya msukosuko wa kifedha unaoikumba klabu hiyo. ***(Mundo Deportivo, via Team Talk)***

**WERNER KUTOONDOKA CHELSEA**

MSHAMBULIAJI wa Ujerumani, Timo Werner mwenye umri wa miaka 25, ana imani kubwa anaweza kubadilisha maisha yake Chelsea na amejitolea kutoondoka Stamford Bridge baada tu ya msimu mmoja, licha ya kuhusishwa kuhamia Borussia Dortmund kama sehemu ya mpango wa makubaliano ya mabadilishano na Erling Braut Haaland. ***(Goal)***

**MAN CITY HAIMTAKI ALABA**

KLABU ya Manchester City haina nia ya kumsajili mlinzi wa Bayern Munich, David Alaba, licha ya kuhusishwa na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28. ***(Manchester Evening News)***

**SARR KUREJEA CHELSEA**

MLINZI wa Ufaransa, Malang Sarr mwenye umri wa miaka 22, atarejea Chelsea akikamilisha muda wake wa kucheza kwa mkopo kule Porto mwisho mwa msimu huu. ***(Record, via Sport Witness)***

**RODRIGUEZ AWANIWA ARSENAL**

ARSENAL wanataka kumsajili kiungo mkabaji wa Real Betis na Argentina, Guido Rodriguez mwenye umri wa miaka 26. ***(Mundo Deportivo via Metro)***

**NACHO AKODOLEWA MACHO**

LIVERPOOL, Juventus na AS Roma zinafuatilia hali ya Nacho kule Real Madrid, huku beki huyo wa Hispania mwenye umri wa miaka 31, akiwa anaingia mwaka wake wa mwisho kwenye mkataba wake. ***(AS)***

HABARI MICHEZO

# MSUVA SASA APANIA KIATU LIGI YA MABINGWA AFRIKA

**Na Adam Fungamwango**

WINGA wa klabu ya Wydad Casablanca ya Morocco na timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars, Simon Msuva, amesema amepania kuwa mfungaji bora wa Ligi ya Mabingwa Afrika inayoendelea.

Akizungumza baada ya mechi ya Taifa Stars dhidi ya Libya mwishoni mwa wiki, ambayo Tanzania ilishinda bao 1-0 lililofungwa na yeye mwenyewe, ikiwa ni mechi ya kusaka tiketi ya kucheza Fainali za Mataifa ya Afrika (AFCON), Msuva alisema lengo lake kubwa msimu huu ni kuibuka kuwa mfungaji bora wa Ligi ya Mabingwa na tayari ameshapachika mabao mawili.

"Mimi kwa sasa nina magoli mawili, anayeongoza ana mabao matatu, kwa hiyo utaona bado nina nafasi nzuri tu ya kuwa mfungaji bora na hilo ndilo lengo langu," alisema Msuva.

Mbali na ufungaji bora, Msuva alisema anataka kuipa timu yake ya Wydad ubingwa wa Afrika ambapo ndiyo malengo yao msimu huu.

"Wydad ni timu kubwa sana Morocco, kama vile unavyoiona Al Ahly ya Misri, Zamalek, au hapa Tanzania Simba na Yanga. Ni timu ambayo lengo lake namba moja ni kuchukua ubingwa wa Ligi Kuu nchini Morocco, halafu kuchukua ubingwa wa Afrika," alisema mchezaji huyo wa zamani wa Moro United na Yanga.

Timu hiyo anayoichezea Msuva, tayari imeshafanikiwa kutinga hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika, ikiwa inaongoza kwenye Kundi C kwa pointi 10, huku Horoya ya Guinea na Kaizer Chiefs zikifuatia zote zikiwa na pointi tano mpaka sasa, kila timu ikicheza mechi nne.

Mchezaji anayeongoza kwa ufungaji mabao mpaka sasa kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika ni Ayoub El Kaabi wa Wydad ya Morocco akiwa na mabao matatu, huku Msuva wa timu hiyo hiyo, Luis Miquissone na Chris Mugalu wote wa Simba wakiwa na mabao mawili kila mmoja.

KITAIFA ZAIDI...



Kiungo wa Yanga, Mukoko Tonombe (katikati), akiwa na wachezaji wenzake wa timu ya Taifa ya DR Congo kwenye chumba cha kubadilishia juzi wakati walipoibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Gambia kwenye mechi iliyopigwa Lubumbashi ya kuwania kufuzu Fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon), zitakazofanyika mwakani nchini Cameroon. **PICHA: MTANDAO**

# Mechi za Yanga, Azam zasogezwa mbele

**Na Saada Akida**

MTENDAJI Mkuu wa Bodi ya Ligi Tanzania (TPLB), Almasi Kasongo, amesema Ligi Kuu Tanzania Bara inatarajiwa kurejea Aprili 8, mwaka huu, kwa kufuata ratiba ya awali huku mechi za Aprili 6 kati ya Azam FC na Mtibwa Sugar na Yanga dhidi ya KMC FC iliyotarajiwa kuchezwa Aprili 7, zikipangiwa tarehe nyingine.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Kasongo alisema awali ligi hiyo ilitakiwa kuendelea Aprili 6 na 7, mwaka huu, lakini imeshindikana kwa sababu ya msiba mkubwa ulioikumba nchi baada ya kufariki dunia kwa aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli, Machi 17, mwaka huu.

Alisema baada ya msiba huo mkubwa, taifa limeingia katika kipindi cha maombolezo kwa siku 21 ambayo yanamalizika Aprili 7, huku mechi ambazo zinatakiwa kuchezwa katika tarehe hizo sasa hazitachezwa na kupangiwa tarehe nyingine.

"Katika ratiba yetu inaonyesha maombolezo ya taifa yanaisha Aprili 7, ambapo kulikuwa na michezo hiyo miwili ambayo itatafutiwa tarehe nyingine, baada ya hapo tutaendelea na ligi yetu kwa kufuata ratiba kwa kuendelea na michezo ya kuanzia Aprili 8 na kuendelea.

"Kabla ya kupata msiba, ratiba ilitakiwa kuendelea Aprili 3 hadi 5 kwa michezo ya Kombe la (Azam Sport Federations Cup) maarufu Kombe la FA hatua ya 16-bora, baada ya kumalizika kwa majukumu ya timu za taifa, hatutaweza tena kuendelea na hiyo michezo na sasa itaangaliwa namna ya kuzipangia tarehe nyingine," alisema Kasongo.

Alisema mechi ambazo zitaendelea Aprili 8, mwaka huu ni Namungo dhidi ya Ihefu mchezo utakaopigwa Uwanja wa Majaliwa mkoani Lindi, pia kutaendelea kwa mechi zingine ikiwamo Yanga dhidi ya Biashara United, utakaopigwa Uwanja wa Benjamini Mkapa jijini Dar es Salaam.

Alisema kuhusu Ligi Kuu ya Wanawake na Vijana , hilo liko chini ya uangalizi wa Shirikisho la Soka Tanzania (TFF).

## Siwa ataja pakuanzia kwa makipa Yanga

**Na Saada Akida**

BAADA ya uongozi wa Yanga, kumtambulisha Kocha mpya wa makipa, Razak Siwa, amesema kadri ya uwezo wake, atahakikisha magolikipa wanakuwa imara, zaidi ili kufikia malengo ambayo wanayotarajia kwenye michezo ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Siwa alisema hana shida na uwezo wa makipa hao kwa sababu amekuwa akiifuatilia Yanga ilipocheza michuano ya Kombe la Mapinduzi pamoja na Ligi Kuu na kubaini pa kuanza kufanyia kazi.

"Sina shida kabisa na makipa waliokuwapo sasa Yanga, wana uwezo mkubwa, kuna vitu ambavyo wanavikosa na mara nyingi nimepata kushuhudia mechi walizocheza na kuona makosa wanayoyafanya, nina imani nitawasaidia na kufikia malengo yetu," alisema Siwa.

Alisema ameona mazingira ya kambi ya timu hiyo, kwa kushirikiana na Kaimu Kocha Mkuu, Juma Mwambusi, watafanya vizuri, hivyo kikubwa ni kuhakikisha wanashinda mechi zao bila kuangalia nyuma, mwenzao anafanya kitu gani.

"Nina imani kubwa Yanga ina nafasi ya kuchukuwa ubingwa endapo tutaungana kwa pamoja na kuhakikisha kila mechi iliyopo mbele yetu tunahitaji kupata ushindi bila kumfikiria anayetukimbiza ameshinda bao ngapi au amepoteza michezo yake," alisema Siwa.

## Jang'ombe yaipania New King Kombe la FA

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

WAKATI timu zilizofanikiwa kutinga hatua ya 16-bora ya michuano ya Kombe la Shirikisho la Soka Zanzibar (FA Cup) zimeendelea kujifua tayari kuelekea kusaka nafasi ya kutinga robo fainali ya mashindano hayo ambayo bingwa hupata nafasi ya kuiwakilisha Zanzibar kwenye Kombe la Shirikisho barani Afrika, timu ya Taifa Jang'ombe imepania kuisambaratisha New King.

Akizungumza na gazeti hili Kocha wa timu ya Taifa Jang'ombe, Mustafa Hassan 'Kocha Muu', alisema amejiandaa kusonga mbele katika michuano hiyo ambayo hatua ya 16-bora inatarajiwa kupigwa Aprili 7, mwaka huu, licha ya kufahamu kwamba ushindani ni mkali hususan kutoka timu za Ligi Kuu.

Taifa Jang'ombe ambayo ipo ligi Daraja la Kwanza Kanda ya Unguja, katika mchezo wake wa FA itakutana na wapinzani wao katika daraja hilo, timu ya New King.

Kuelekea mchezo huo, Kocha Mkuu, alisema anaifahamu vema New King na ni timu ngumu na kwamba licha ya kuwafunga katika michezo ya ligi ambayo wamekutana, anaamini wapinzani wao hao watajipanga ili wasirejee makosa waliyoyafanya awali walipokutana.

# Michezo

Jumatano Machi 31, 2021

Nipashe




AGUERO AGEUKA LULU BARCA, JUVE NA PSG

HABARI UK 22

TUPO TAYARI...



Wachezaji wa Yanga, kiungo Zawadi Mauya (kushoto) na beki Kibwana Shomary wakiwa mazoezini Kigamboni, Dar es Salaam juzi, kujiandaa na Ligi Kuu Bara ambayo inatarajiwa kuendelea Aprili 8, mwaka huu, baada ya kumalizika kipindi cha maombolezo ya aliyekuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. John Magufuli. **MPIGAPICHA WETU**

## YANGA YAIMARIKA, MAJERUHI WAREJEA

**Na Mwandishi Wetu**

KIKOSI cha Yanga kimezidi kuimarika baada ya nyota wawili waliokuwa majeruhi, Mapinduzi Balama na Dickson Job, kuimarika na kuanza kufanya mazoezi, imeelezwa.

Job alikuwa anasumbuliwa na majeraha ya nyama za paja ambayo aliyapata kwenye timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars na tayari amerejea kwenye ubora wake na kuanza mazoezi.

Kwa upande wa Balama, ambaye alikuwa nje kwa muda mrefu akitibu majeraha ya kisigino aliyoyapata msimu wa 2019/20 wakati wa maandalizi ya mchezo wa Ligi Kuu Bara dhidi ya Ndanda FC naye ameanza programu maalum ambayo muda si mrefu itamfanya kurejea uwanjani.

Kaimu Kocha Mkuu wa Yanga, Juma Mwambusi, amemwambia mwandishi wetu kuwa maendeleo ya nyota hao ambao walikuwa wakisumbuliwa na majeraha kwa sasa yamezidi kuimarika.

"Taratibu wale ambao hawakuwa fiti wanarudi, Mapinduzi Balama amepewa program maalum huku wachezaji wengine wakiwa wameanza mazoezi.

# MIQUISSONE, KAGERE WAMTIBULIA GOMES

●●●Ni katika mipango ya kuivaa AS Vita Jumamosi kwa Mkapa, sasa awataka kuhakikisha wanawasili kikosini kabla ya...

**Na Saada Akida**

WAKATI mazoezi ya kikosi cha Simba kujiandaa na mechi ya Ligi ya Mabingwa Afrika hatua ya makundi dhidi ya AS Vita yakizidi kupamba moto, wachezaji wawili wa mabingwa hao wa Tanzania, Luis Miquissone na Meddie Kagere ndio wanaochelewesha mipango ya miamba hiyo ya soka nchini, imeelezwa.

Simba ambayo ipo kileleni mwa msimamo wa Kundi A katika michuano hiyo ikiwa na pointi 10 ikifuatiwa na mabingwa watetezi, Al Ahly ya Misri yenye alama saba, Jumamosi itaikaribisha AS Vita ya DR Congo yenye pointi nne katika Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Katika mechi hiyo, Simba itakuwa ikihitaji sare tu ili kufuzu hatua ya robo fainali, wakati AS Vita yenyewe ikihitaji ushindi ili kujiweka katika nafasi ya kufuzu hatua hiyo, wakati huu Al Ahly ambao watakuwa ugenini dhidi ya vibonde wa kundi hilo, Al-Merrikh ya Sudan yenye alama moja, nayo ikihitaji ushindi huku ikiombea Wekundu wa Msimbazi hao washinde ili nao wakate tiketi kabla ya mchezo wa mwisho.

Kuelekea mchezo huo, Kocha Mkuu wa Simba, Didier Gomes, amesema anawakosa mapema katika maandalizi nyota hao wawili, Miquissone na Kagere, ambao jana walikuwa wakimalizia majukumu yao na timu za taifa kwenye mechi za kuwania kufuzu Fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon), zitakazofanyika mwakani nchini Cameroon.

Hivyo, Gomes ametuma ujumbe akiwataka Miquissone na Kagere kuhakikisha ifikapo kesho, Alhamisi wawe wameungana na wenzao kambini ikiwa ni siku mbili kabla ya kuivaa AS Vita.

Miquissone yupo na timu ya Taifa ya Msumbiji ambayo jana ilikuwa ikiikaribisha Cape Verde wakati Kagere yeye alikuwa na kikosi cha timu ya Taifa ya Rwanda nchini Cameroon wakivaana na wenyeji hao.

Gomes alisema wako makini katika kuhakikisha wanafanyia kazi kasoro ndogo ndogo zilizojitokeza katika mechi zilizopita, lakini kukiandaa kikosi chake kulingana na ubora wa AS Vita ambao anaamini watakuwa na mbinu kali wakati huu wakisaka pointi tatu kwa nguvu ili kujiweka katika mazingira mazuri ya kufuzu robo fainali.

Alisema ni mechi muhimu sana kwao kuhakikisha wanapata pointi muhimu kwa ajili ya kusonga mbele kucheza robo fainali ya michuano hiyo kwa kuendeleza ushindi katika mechi zao hizo za makundi.

"Tunahitaji kupambana kuhakikisha tunafanya vizuri katika michezo miwili, ikiwamo dhidi ya AS Vita, tutakaocheza nyumbani, lengo ni kushinda na kutinga robo fainali," alisema Gomes.

Naye Meneja wa Simba, Patrick Rweyemamu, alisema jana jioni wachezaji wote waliokuwa na timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars wameungana na wenzake huku baadhi yao walikuwapo katika mataifa yao wakitarajiwa kuungana na wenzao leo isipokuwa Miquissone na Kagere.

Alisema Miquissone na Kagere wao wataripoti kambini Alhamisi kwa sababu timu zao za taifa zilikuwa na mechi jana.

"Maandalizi yanaendelea vizuri na tunatarajia hadi Alhamisi timu imekamilika kwa wachezaji wakigeni ambao walikuwa katika majukumu ya timu ya taifa kurejea katika klabu na kuendelea kupambania timu kufikia malengo yetu ya kuhakikisha tunapata ushindi ambao utatuhakikishia kucheza robo fainali," alisema Rweyemamu.

Kikosi cha Simba kinaendelea na mazoezi katika Uwanja wa Simba Mo Arena uliopo Bunju, Dar es Salaam.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002